SUPA JACKPOT
TZS. 1,152,911,993
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



RIPOTI YA UCHUNGUZI
**Dada** wa kazi wanavyotumika ulaji mabilioni mikopo ya 10%

UKURASA 4


Anayetaka kubebwa kama jeneza mwacheni abebwe!
Ukurasa 13
BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 15, 2023 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
SIKU YA TAIFA YA BIMA Msimamizi Mkuu wa fani aorodhesha mafanikio, apiga debe wakati umetimu kuwapo Bima Kilimo
Ukurasa 12
SAFARI YA 'KILIMO CHA KUFA NA KUPONA'
Sekta kilimo inavyobaki mtaji Taifa tangu zama za Mwalimu hadi Samia
Na Mwandishi Wetu

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Septemba 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581434
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Samia awafunda majaji utoaji haki

• **Aonya** fedha za hongo zitawaponza hadi kwa Mungu... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Abdul-Hakim Ameir Issa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Takwimu unywaji pombe Tanzania zatikisa Afrika

UKURASA 3



Mnyika Mutungi

## Msajili ajibu hoja sita za CHADEMA

UKURASA 3

MICHEZO GAMONDI AWAFUNGIA KAZI NYOTA 8 AL MERRIKH UK.24
KATUNI UK.6

## Mama adaiwa kufanya njama mwanafunzi aliyebakwa, kutoroshwa

**Na Prosper Makene**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kinondoni linachunguza sakata la mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mchanganyiko mwenye umri wa miaka 17, anayedaiwa kubakwa na kutoroshwa na mwanamume kwa miezi miwili.

Ni baada ya baba mzazi wa mtoto huyo, Haji Khamara, kudai jeshi hilo kutofanyia kazi suala hilo tangu mwanawe alipotoweka mwezi Juni mwaka huu nyumbani kwao Kigamboni, Dar es Salaam na kupatikana mwezi uliopita.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kinondoni, Gabriel Mukungu, akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, alimtaka mzazi wa mwanafunzi huyo kufika ofisini kwake haraka ili jeshi limsaidie katika kesi hiyo.

"Kesi zote zipo hapa chini yangu, hivyo tunaomba Bwana Haji aje kunipa kesi yake, ishughulikiwe na kitengo changu," alisema Mukungu.

Khamara alidai jana kuwa ameshamwandikia barua Mkuu wa Jeshi la Polisi kumwomba amsaidie haki itendeke.

"Nimemwandikia barua IGP kuomba msaada wa Jeshi la Polisi katika kesi hii, hivyo na ninyi watu wa vyombo vya habari ninaomba mnipazie sauti yangu nipatiwe msaada kwa mtu huyu aliyembaka binti yangu afikiswe katika vyombo vya sheria," alidai.

Pia alidai kuwa mama wa mtoto huyu alihusika kumtorosha binti yake ili kuzuia mwanamume aliyembaka kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Baada ya kuweka mitego na kumkamata, binti yangu alinieleza kuwa mama yake ndiye alihusika kumtorosha nyumbani akishirikiana na huyo jamaa aliyembaka na kwenda naye maeneo ya Salasala, jijini Dar es Salaam ambako tulimkamata," alidai.

Abeid Kamugisa, Mkuu wa Shule ya Sekondari Mchanganyiko alisema binti huyo hajaonekana shuleni tangu Juni mwaka huu. Alishauri polisi wachukue



Wahitimu wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Mkimbizi, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, wakifurahia baada ya kumaliza mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Samia awafunda majaji utoaji haki

**Jenifer Gilla na Antoni Manjoro** (TUDARCo)

Rais Samia Suluhu Hassan amewataka majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kusimamia haki za wananchi na kuonya upindishaji kwa tamaa ya fedha, ambazo hata wakijenga nyumba za kifahari watakufa na kuziacha na kuishia kubeba mizigo ya dhambi.

Pia, amemwagiza Naibu Mwanasheria Mkuu, Prof Kennedy Gastom, kumsaidia Mwanasheria Mkuu kuhakikisha serikali haiingii kwenye matatizo ya kisheria ikiwamo ya uwekezaji na ukiukwaji wa mikataba.

Rais Samia alitoa maelekezo hayo jana wakati akiwaapisha viongozi hao Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya kuwateua na kuwasisitiza wakati wanatekeleza majukumu yao kuzingatia maridhiano, ustahamilivu, kubadilika na kujenga taifa.

Alimtaka Prof. Gastom kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, zikiwamo taasisi hizo zisomane kwa kuimarisha utendaji kazi, vitendea kazi na mazingira rafiki.

Akizungumzia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Rais alimwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Balozi Stephen Mbundi na Naibu Katibu Mkuu wake Balozi Said Mussa, kuhakikisha utekelezwaji wa shughuli za Afrika Mashariki unapewa uzito.

Pia, umuhimu wa kushirikiana na tume aliyoiunda kuchunguza wizara hiyo, ili waje na mapendekezo ya kuiboresha katika kukuza diplomasia ya uchumi, kualika wawekezaji na kutanua biashara.

Alisema kuongeza majaji pekee hawatoongeza ufanisi katika mhimili huo, kama hawatokuwa na utayari wa kuifanya kazi kwa weledi na kuwasisitiza wajizatiti kuleta mabadiliko na kuahidi kuwa serikali ipo tayari kutoa msaada kwa mahakama zisimame imara na kutenda haki.

"Tumaini letu lingine ni kujenga imani ya mahakama kwa wananchi, kutoa haki kuendana na mashauri yanayoletwa. Mwenye haki apate haki, asiye na haki basi aambiwe huna haki, mwenye haki ni huyu," alisema Rais Samia.

Alisema uapisho huo umekuja muda mfupi baada ya Tume ya Haki Jinai aliyoiunda kuwasilisha ripoti yake inayoonyesha kuna kazi kubwa ya kufanya ikiwamo kuimarisha teknolojia, miundombinu na nguvukazi katika mahakama.

Alisema jinsi nchi inavyokua kiuchumi na kisiasa, mahakama pia inahitaji kukua, hivyo atakuwa anaongeza watendaji katika mhimili huo kadri uchumi utakavyoruhusu.

Alitaja sababu ya kuchagua majaji wa Mahamaka Kuu wenye umri mdogo kuwa anataka wafanye kazi kwa muda mrefu na kuipunguzia serikali mzigo wa kuajiri watu wapya na kulipa mafao ya wastaafu ndani ya muda mfupi.

Aliwaagiza naibu katibu na makatibu kufanyakazi kwa weledi; "basi nikigundua kuna hivi na vile, Zuhura anawahusu na yeye (Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu) huwa anarusha saa nane usiku, alfajiri ukiamka hamna kitu, sasa tusifike huko, nendeni kawajibikeni," aliagiza.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alimshukuru Rais Samia kwa kuwaongeza nguvu katika mahakama hiyo kwa kuwa tangu aingie madarakani ameteua jumla ya majaji wa Mahakama ya Rufani 19 wakati Mahakama Kuu ameongeza majaji 63 na kuifanya kuwa na jumla ya majaji 105.

Alisema idadi hiyo itaongeza kasi ya kusogeza huduma ya utoaji haki kwa wananchi nchini na kuwapunguzia kadhia ya kutembea umbali mrefu na kusubiri kwa muda mrefu uamuzi wa majaji hao.

Alisema serikali inafanyia kazi changamoto hiyo na sasa inajenga mahakama hizo katika mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Pwani, Geita, Simiyu, Njombe, Singida Songwe, Katavi na Pemba.

Alisema kwa kipindi cha miaka saba walikuwa na mashauri 99 yaliyohusu utovu wa nidhamu katika tume na kati ya hayo, 33 walifutwa kazi, 13 walipewa onyo, 38 walistaafishwa kwa manufaa ya umma na 15 walirejeshwa kazini.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwapongeza viongozi walioapishwa na kuwasihi kufanya kazi kwa kuzingatia weledi, uaminifu, uadilifu na dhamira ya dhati ya kutenda haki kwa wale wote watakaokwenda kwao kutaka msaada.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, alimshukuru Rais Samia kwa hatua mbalimbali anazochukua kuboresha huduma ya kutoa haki kwa wananchi. Bunge linaelewa dhamira hiyo ni njema kwa nchi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
15.09.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatatu tarehe **18-09-2023 hadi 21-09-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero** kupitia **Mikumi,** gari hizo zina namba za usajili: **T 204 DYJ / T 887 DJB T 478 ECF / T 837 DJB T 980 EDR / T 630 AJA T 988 EDR / T 272 DUH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu** - **mita 21.00**
**Upana** - **mita 5.00**
**Kimo** - **mita 5.20**

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

117601002

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
15.09.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe **19-09-2023 hadi 22-09-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kinyerezi Power Plants** kupitia Tabata, Segerea hadi Kinyerezi, gari hizo zina namba za usajili: **T 308 EAG / T 684 EBP T 133 CCP / T 232 ABE**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu** - **mita 31.00**
**Upana** - **mita 3.50**
**Kimo** - **mita 6.00**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port, hadi Kinyerezi Power Plants** kupitia Tabata, Segerea hadi Kinyerezi gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

117601002

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

HABARI KITAIFA

# Takwimu unywaji pombe Tanzania zatisha

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Afya imesema takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania inaongoza kwa matumizi ya pombe Afrika huku watu wenye umri wa kuanzia miaka 15, wanatumia wastani wa ndoo moja ndogo kwa mwaka.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza (NCD) kutoka wizara hiyo, Dk. Omary Ubuguyu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano uliohusisha wahariri wa vyombo vya Habari.

Mkutano huo uliolenga kujadili nafasi ya vyombo vya habari katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, uliandaliwa na Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA) na Chama cha Wagonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA) kwa ushirikiano wa wizara na Taasisi ya PhamAccess.

Wakati akitaja vitu ambavyo ni kichocheo cha magonjwa yasiyoambukiza, Dk. Ubuguyu alisema pombe ni chanzo kikuu huku akibainisha kuwa mwaka 2012 asilimia 29 ya Watanzania walikuwa wanakunywa pombe na zaidi ya asilimia 24 wakiwa ni wanaume ambao walionekana kunywa kwa kiwango kikubwa.

"Hiki si kipimo kikubwa cha pombe. Kipimo kikubwa ni kwa kiwango gani taifa hili linatumia pombe ili kusema matumizi ni kiwango cha kawaida au kiwango kilichokithiri.

"Kwa Tanzania ukiangalia takwimu, hata juzi zilitoka kwamba inaongoza Afrika. Kwa wastani, kwa mwaka ni kiwango cha unywaji kwa mwaka ni lita 9.1 (sawa na ndoo ndogo ya lita 10) wakati kiwango kwa Afrika ni lita sita. Sisi tuko juu kwa lita 3.1 zaidi," alisema.

Dk. Ubuguyu alitaja kichocheo kingine cha magonjwa hayo ni kutofanya mazoezi lakini mwaka 2012 waligundua watu wengi wanafanya. Kwa wakati huo, alisema waliokuwa wanafanya kwa ajili ya afya zao walikuwa asilimia sita tu na wengine ulikuwa ni ugumu wa maisha na si kuwa na nidhamu ya kujenga afya.

Mtaalam huyo alitaja kichocheo kingine ni suala la lishe ambapo asilimia 2.5 tu ya watu wote ndiyo waliokuwa wakitumia matunda na mboga za kutosha.

"Kichocheo kingine ni matumizi ya tumbaku ikiwamo shisha. Lakini katika magonjwa yasiyoambukiza kuna changamoto kubwa sasa hivi imeingia ya bodaboda na ajali. Nidhamu barabarani iko chini," alisema

Alisema utafiti mwingine uliofanyika mwaka 2016 kuangalia hali na viashiria vyake shuleni kwa kuangalia ufanyaji mazoezi ilibainika kuwa kwa watoto hali ilikuwa mbaya kwa kuonyesha kuwa asilimia 20 tu wanafanya.

"Hawa watakapofika umri wa miaka 40 na kuendelea, hali itakuwa mbaya zaidi. Matumizi ya vinywaji baridi na vyenye sukari nyingi kwa watoto wetu ni asilimia 45.

"Hali ya afya ya akili ikabainika asilimia 10 ya vijana wana uhatarishi wa kujiua. Mtoto mmoja katika watoto 10 wanawaza kujiua na kati yao mmoja aliwahi kufanya jaribio hilo la kujiua. Tunazungumza haya ili tuone namna ya kuyabeba," alisema..

Mwenyekiti wa TDA, Prof. Andrew Swai, alisema:

"Mwaka 1991 tulifanya hesabu tukaona kama ni kuwatibu wagonjwa wenye kisukari peke yake itahitaji asilimia tisa ya bajeti yote ya serikali kwa wakati huo.

Dk. Alphoncina Nanai kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), alisema takwimu za mwisho za dunia za 2006 na 2008 zinaonyesha vifo milioni 31.4 kati ya milioni 41 vimesababishwa na magonjwa yasiyoambukiza .


NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street
P. O. Box 6707
Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045
Fax: +255 22 2112045

Dev Recoveries Ltd

MAUZO KWA NJIA YA ZABUNI

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED** ya tarehe 04/09/2023, kampuni yetu imepewa maelekezo ya kuuza dhamana kwa njia ya zabuni kama dhamana inavyoanishwa hapo chini:
Dhamana ni ghorofa ya tisa kwa ofisi/Apartment lenye ukubwa wa mita za mraba 1441 iliyopo **KITALU NO 2423/208, HATI NAMBARI 102095/10, L.O NO. 632183 ENEO LA KISUTU, MANISPAA YA ILALA, DAR ES SALAAAM.**

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA KWA ZABUNI:**

**MASHARTI YA ZABUNI**

1. Mzabuni yoyote anakaribishwa kuleta zabuni kwa ajili ya kununua kwenya bahasha itakayoonyesha ofa yake na anuani ya mzabuni na iwekwe na anuani inayoonyesha hapo chini kabla ya saa Saba (07:00) mchana tarehe 05/10/2023 kwenye ofisi inayoelelzewa hapo chini. Wazabuni mnakaribishwa uwepo wenu wakati wa kufunga zabuni kama utakuwa na nafasi.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia baada ya siku nne ya ushindi wa zabuni 25% ya bei aliyoshinda zabuni na kiasi cha pesa kilichobaki mnunuzi atalipa ndani ya siku kumi na nne au kama atakavyokubalian na benki muda wa kulipa kiasi kilichobaki.
3. Gharama za kubadilisha hati miliki na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
6. Kwa mawasiliano zaidi piga simu No: 0782 065 914 / 0712 073 680

**MKURUGENZI MKUU**
**DEV RECOVERIES LIMITED**
**NIC LIFE HOUSE, 4TH FLOOR, WING C, SOKOINE DRIVE/OHIO STREET**
**PO BOX 6707, DAR ES SALAAM**

117601402


# Msajili ajibu hoja sita za CHADEMA

**Na Halfani Chusi**

MSAJILI wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi amekijibu Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kupinga dai lake kwamba maazimio 15 ya wadau wa vyama vya siasa vilivyokutana wiki hii, yalinuia kuibeba serikali.

Jaji Mutungi aliiambia Nipashe jana, akipinga hoja sita alizozitoa Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, akidai maazimio hayo ni njama nyuma ya pazia, serikali inashirikiana na vyama vya siasa kuhalalisha sauti ya kambi ya upinzani.

Kwa mujibu wa Mnyika aliyezungumza na Nipashe awali, wana hoja sita akizitaja hawakubaliani na serikali kupitia maazimio tajwa.

Aliorodhesha hoja zake kwamba maazimio hayo 15 yamekiuka madai yao ya: Kupinga ajenda ya kutolewa elimu ya Katiba, haja ya kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, polisi kuingilia uchaguzi, kukabili rushwa kipindi cha uchaguzi, kuchelewa mchakato wa Katiba Mpya na kutokuwapo ratiba maalum kwa vyama vya siasa kuwasilisha hoja zao.

Kwa mujibu wa Jaji Mutungi, vyama vile ambavyo vimeafikiana kwa serikali, bado si maazimio mpaka watakapozikabidhi rasmi. Alifafanua kwa kauli ya kung'aka kuwa: "Na kama vipi wanaweza wakaja kuthibitisha kama tutakayoyakabidhi serikali, je yatakuwa na tofauti na hayo?

"Si ajabu ukute yamefika 20 au 30, lakini ninaomba ieleweke mpaka siku tutakapokabidhi hayo maazimio serikalini.

"Tutatoa maazimio rasmi, yale ya jana ilikuwa ni katika kufunga mkutano lazima yasomwe tu kama tukio la kuhitimisha, kwa sababu huo mkutano ulikuwa unapelekea maazimio serikali sasa tutakapokuwa tunakabidhi rasmi tutatoa taarifa."

Mnyika aliyezungumza na Nipashe awali, alilalamika kwamba, sababu za CHADEMA kutohudhuria mkutano huo uliofunguliwa Jumatatu wiki hii na Rais Samia Suluhu Hassan , akitoa sababu haikuwa na imani nao, pia Baraza la Vyama vya Siasa la siku tatu, halikuwa na uwezo kujenga mwafaka unaostahili.

Mkutano huo ulifungwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Mnyika, chama chake kilikuwa na shaka, ambalo limejidhihirisha kutokana na maazimio yao 15 ambayo aliyafafanua hayana uzito kama ilivyokuwa kwa yale 21 yaliyopendekezwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD).

"Nitakupa mfano wa mambo machache, mkutano ule wa TCD uliazimia mchakato wa katiba uendelee kwa serikali kupeleka bungeni muswaada wa sheria ambayo itaweka ratiba na namna ya kuendelea na mchakato wa katiba.

"Lakini mkutano huo wa serikali haujaweka kabisa azimio la kupeleka muswada wa sheria bungeni kwa ajili kuendeleza mchakato wa katiba, badala yake wamepitisha azimio Rais aunde kamati kuhusu mchakato wa katiba," alilalamika Mnyika.

Alisema kitendo cha kupitisha azimio hilo, bila kupinga uamuzi wa serikali kuhusu kutolewa elimu ya katiba kwa miaka mitatu kimsingi wanatengeneza mazingira ya mchakato wa katiba.


HELD UNDER THE PATRONAGE OF HON. DR. DOTO MASHAKA BITEKO (MP), DEPUTY PRIME MINISTER AND MINISTER FOR ENERGY, MINISTRY OF ENERGY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

ENDORSED BY MINISTRY OF ENERGY

Tanzania Energy Congress
20 - 21 September 2023 | Dar Es Salaam, Tanzania

INVESTING IN TANZANIA'S SUSTAINABLE ENERGY ECONOMY

WITH THANKS TO OUR 2023 SPONSORS & PARTNERS TO DATE

DIAMOND SPONSOR: PANAFRICAN ENERGY an Orca Company
PLATINUM SPONSOR: equinor
SILVER SPONSORS: EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE, TotalEnergies
BRONZE SPONSORS: AGL, CRDB BANK, MAUREL & PROM, NEWAY, NMB, ORYX ENERGIES, PBZ BANK, slb
ENERGY TRANSITION PARTNER: Songas
COUNTRY PARTNER: OMAN ISFS eMarketplace
KNOWLEDGE PARTNER: Hawilti
ICT PARTNER: tigo business
BRANDING PARTNER
SUPPORTING PARTNERS: ewura, ZPRA
ORGANISED BY: dmg events

BOOK YOUR DELEGATE PASS TODAY

Contact JAYSON ESTRADA on +255755030622 or Email: info@tanzaniaenergycongress.com

tanzaniaenergycongress.com #TanzaniaEnergyCongress

217593902

**RIPOTI YA UCHUNGUZI-2**

## MIKOPO YA ASILIMIA 10

# Dada wa kazi wanavyotumika katika ulaji mabilioni ya umma

Na Mwandishi Wetu

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na malalamiko ya wajasiriamali dhidi ya vitendo vyenye viashiria vya rushwa katika utoaji mikopo ya halmashauri kwa makundi maalum nchini, maarufu mikopo ya asilimia 10. Endelea kufuatilia kujua undani wa suala hili**

MKURUGENZI Mkuu wa asasi inayojihusisha na wajasiriamali wanawake wanaofanya biashara katika masoko ya Equality For Growth (EFG), Jane Magigita, anabainisha kuwapo idadi ndogo ya wanawake toka kundi hilo walionufaika na mikopo ya halmashauri.

Anataja vikwazo dhidi ya kundi hilo vinajumuisha kutokidhi masharti ya kupatiwa mikopo, hasa ulazima wa kuwa na kikundi kilichosajiliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ni vigumu kwao kuunda kikundi na watu wasiofahamiana vizuri. Wanakutana sokoni.

Jane anataja ugumu mwingine kwa wajasiriamali hao kupewa mikopo hiyo ni ushiriki wa wanasiasa (wenyeviti wa mitaa na madiwani). Anadai wana nguvu ya nani apate nani asipate.

"Mara nyingi wanawapa wanachama wa vyama vyao zaidi. Wale ambao sio wafuasi wao hawapewi. "Shida nyingine kwa wajasiriamali wadogo ni sharti la kuwa na andiko. Wengi hawajui kuandaa andiko la mradi. Wanatafuta makanjanja na vishoka, wanawalipa hata kama hawana uhakika wa mkopo.

"Hii ni kwa sababu wanawake wengi hawana elimu ya ujasiriamali. Wazo analo, lakini hajui namna ya kuliweka katika maandishi," Jane anafafanua.

Jane pia ana angalizo kwa serikali kwamba kusudio la kuja na utaratibu mpya wa kupitishia mikopo hiyo benki, lizingatie atakayebeba riba ili makundi lengwa yafikiwe pasi na vikwazo vya kibenki.

**UDANGANYIFU ULIVYO**

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Kinondoni, Alex Tiboneka, anawanyooshea kidole watendaji wa serikali za mitaa ambao huwatambulisha waombaji feki wa mikopo na pale ofisi yake inapojaribu kuhoji, anaonekana anataka rushwa na hivyo kuingia katika mgogoro.

"Utapeli unafanywa na wale wenye uelewa mkubwa. Wakati mwingine tunapokea maombi mtu ana barua ya serikali za mitaa 'ninamtambulisha fulani kutoka shina namba fulani, ni mkazi wangu'.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa.

"Mwenyekiti wa Mtaa akishamtambulisha, mimi nikimkataa, yanaibuka maswali 'kwanini huyu anamkataa wakati mimi nimeshamtambulisha? Wewe ni nani hadi ukatae?'

"Wakati mwingine tunafuatilia mwenyekiti anamtambulisha mtu ambaye si mkazi wake. Tuliwahi kwenda eneo moja (hakulitaja) mtu anaonesha hapa ni kwetu, lakini yeye mwenyewe anaishi Kibamba," anafafanua.

Tiboneka anabainisha mbinu nyingine inayotumika ni pale mtu anaomba mkopo akiwa na wenzake wanne, lakini ameshawaambia wao watakuwa wadhamini na mkopo ukitoka anawagawia kidogo na kiasi kinachobaki anatumia mwenyewe.

"Kwa vijana, tulikutana na kikundi kimoja tunawadai marejesho. Wanatueleza waliambiwa wao ni wadhamini tu. Unakuta mtu ana njaa sana, hajawahi kushika fedha nyingi, anapewa Sh. 100,000 anakubali kuwa sehemu ya kikundi, kumbe kafanywa mdhamini tu," anasema.

Kwa vikundi vya wanawake, Tiboneka anabainisha wapo 'wajanja' wanaotumia watu wengine kujipatia mikopo, hivyo kuwanyima fursa wasio na uelewa.

"Imefika mahali, wapo wanaotumia hadi wasichana wa kazi, unakuta mtu ana wasichana wa kazi wawili na watoto wake wawili, jumla watano. Wanatengeneza kikundi anakisajili. Mkopo ukishaingia anamfukuza msichana, anabaki na watoto wake ambao baadaye wanakwenda shuleni, anabaki peke yake akitumia mkopo. Haya mambo tunakutana nayo sana.

"Unakuta iliingia Sh. milioni 50, halafu mama ndiye kiongozi wa kikundi, wasichana kawafukuza na watoto wako shuleni. Mazingira kama haya tumekutana nayo. "Kwa vikundi vya watu wenye ulemavu, unakuta mmoja ni mwelewa sana. Anakuja mnampa maelekezo mengi anaelewa. Na tunamwambia 'mwongozo lazima muwe wawili'.

"Akitoka anamwangalia anayemmudu 'anamwimbisha'. Mwingine unakuta ni mlemavu hata kutembea hawezi, anahakikisha anamfikisha ofisini, baada ya fedha kutoka haonekani," anafafanua.

Ofisa huyo anaanika mbinu nyingine za ulaji wa mabilioni hayo ni pale "mtu mwenye nguvu" kuwa nyuma ya kikundi cha vijana. Anawasaidia hadi wanapata mkopo, lakini miamala inapopatikana, kuna fungu wanapaswa kumpatia.

"Unaweza kumtafuta kwenye miamala iliyofanyika, lakini humwoni kokote. Unawatafuta walete rejesho hawaleti, ilifikia hatua hatuwapi fedha taslimu bali tunaangalia mahitaji ya mradi ndiyo tuwapatie. Kwa mfano, wanataka kufungua kiwanda cha kufyatua matofali, wanaleta 'invoice' (ankara za malipo), tunalipa dukani.

"Tunakumbana na changamoto nyingi sana. Ukitega hapa anategua pale. Ukiziba hapa anatoboa pale. Tunahangaika na watu wenye akili nyingi za kutaka kujipatia hizi fedha kwa ujanja," anasema.

Tiboneka anataja hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani, akishauri vijana kuepuka kutumiwa na wajanja wachache, akiwa na tahadhari baadhi yao wanapopandishwa kizimbani, wanapohojiwa wanadai hawajui lolote kwa kuwa fedha zilichukuliwa na mwenzao mmoja.

"Tuliwahi kumkamata mmoja, ilibidi tumrekodi kupata ushahidi sahihi. Alitueleza kuwa mjumbe wa serikali za mitaa aliwaambia waseme 'yule msichana wa kazi ameshafariki dunia' kumbe baada ya fedha kuingia alimfukuza. "Ilibidi hawa tunaowakamata tunawafundisha namna ya kuwarekodi waliowatumia kupata mikopo hii. Imetusaidia kuwanasa. Kwa kiasi kikubwa utapeli unafanywa na baadhi ya watu ambao sio waaminifu," anasema.

Mwandishi wa habari hizi alipohitaji ufafanuzi kuhusu utolewaji wa mikopo hiyo katika Manispaa ya Temeke toka kwa Meya wa Manispaa hiyo, Abdallah Mtinika, alisema mikopo inatolewa kulingana na mwongozo. Wametoa mikopo kwa vikundi vya kilimo, mifugo, mazingira, maji na afya. Pia kwa wajasiriamali wadogo wenye magenge ya matunda, mboga, vitafunwa na maduka ya nguo.

Mtinika anataja vikwazo vilivyopo ni wakopaji kutorejesha kwa wakati, migogoro katika vikundi kutokana na maslahi binafsi, fungu dogo kwa ajili ufuatiliaji, vikundi kutekeleza miradi ambayo hawana uzoefu nayo na dhana ya kuchukulia mikopo hiyo ni msaada.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018/19 hadi Aprili mwaka huu serikali ilipotangaza kusitisha mikopo hiyo, halmashauri ilikuwa imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 14 kwa vikundi 833 vinavyoundwa na watu 7,720 kutoka kata zote 23 za manispaa hiyo. Kati yao, wanawake ni 4,023, vijana 2,577 na wenye ulemavu 1,020.

Mnamo Machi 7 mwaka huu, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Amani Mafuru, alitoa taarifa kuhusu mikopo hiyo, akibainisha kuwa hadi Juni 2022, zaidi ya Sh. bilioni 23.4 zilishatolewa kwa vikundi 1,963 vyenye wanufaika 19,800 jijini.

Mafuru alifafanua kuwa kati ya fedha hizo, mapato ya ndani yalikuwa Sh. bilioni 19.9 huku Sh. bilioni 5.5 zikiwa ni fedha za marejesho ya mikopo hiyo.

Tovuti rasmi ya Manispaa ya Kinondoni inaonyesha mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 3.9 ilitolewa katika robo ya nne ya mwaka 2021/22 kwa vikundi 286. Mgawanyo wake ni wanawake vikundi 182, vijana (90) na wenye ulemavu (14).

Vilevile, tovuti rasmi ya Manispaa ya Temeke inaonyesha jumla ya Sh. bilioni 4.6 hadi Machi mwaka huu, zilikuwa zimetolewa kwa vikundi 185 vyenye wanufaika 1,146.

*ITAENDELEA KESHO



Tangu 2018/19 hadi Aprili 2023, Sh. bilioni 14 zimekopeshwa kwa vikundi 833 wilayani Temeke.

## TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua zichukuliwe dhidi ya wanaoingiza watoto harusini

**KATIKA** jamii ya Kitanzania kumekuwa na matukio mengi zikiwamo sherehe za kuwaaga mabinti kwa ajili ya kuanza maisha mapya ya ndoa, pamoja na harusi ambazo ni lango la vijana wanaoondoka mikononi mwa wazazi wao ili kuanza maisha mapya ya mke na mume.

Sherehe hizo hupambwa na burudani mbalimbali kama vile muziki wa kileo, injili na shoo mbalimbali zinazofanywa na wasanii, wageni waalikwa na ndugu wa familia. Yote hiyo ni kwa ajili ya kufurahia tukio lililojiri ndani ya jamii likiwahusisha ndugu jamaa na marafiki.

Hata hivyo, katika baadhi ya matukio hayo ya harusi na 'sendoff', kumekuwa na shoo na burudani za muziki zinazowahusisha watoto. Katika sherehe hizo ambazo nyingi hufanyika usiku, watoto hupewa nafasi ya kucheza shoo za muziki na wakati mwingine hutunzwa fedha. Wakati mwingine, watoto hao huingia katika kumbi za sherehe hizo kwa miondoko inayowafanya watu kufurahi, yote hiyo ni katika kupamba tukio lionekane la kufana.

Hivi karibuni mathalan, kuna video ilisambaa kwenye mitandao mbalimbali ikionyesha watoto wakitoa burudani kwenye sherehe wakati wa usiku na katika Miondoko isiyofaa kwa umri wao. Video hiyo ilimwibua Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, na kuwatafuta wazazi wa watoto hao huku akikemea kitendo hicho.

Waziri Gwajima, kutokana na kukerwa na kitendo hicho, alipiga marufuku watoto kushiriki sherehe zinazofanywa usiku huku akiwataka washereheshaji na jamii kuzingatia sheria inayokataza udhalilishaji dhidi ya watoto.

Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 (iliyorekebishwa Mwaka 2019), kifungu cha 158 (1) (c) inazuia kumtumia mtoto kwenye maonesho ya harusi, mitindo ya nguo au maonesho mengine kama hayo nyakati za usiku. Sheria hiyo inabainisha kuwa mtu yeyote atakayebainika kuikiuka, adhabu yake ni faini ya Sh. 500,000, au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Tukio hilo ambalo video yake imesambaa ikionyesha utumikishwaji na udhalilishwaji wa watoto, ni moja ya matukio mengi ambayo yametamalaki katika jamii za Kitanzania hasa nyakati za sherehe. Katika hali ya kawaida, matukio kama hayo yanaonyesha kuwa hayana madhara lakini ukweli ni kwamba kuna athari kubwa kama yataachwa bila kukemewa na hatua kuchukuliwa.

Dk. Gwajima anastahili pongezi kubwa katika kuibuka na kukemea kitendo hicho huku akitoa maagizo kwa wadau mbalimbali kuchukua hatua. Kama alivyosema, ni wakati sasa kwa washereheshaji na wamiliki wa kumbi zinazotumika kwa sherehe hizo kuchukua hatua kwa kuwakataza wahusika kutoingiza watoto kwenye shughuli hizo.

Vyombo vya ulinzi na usalama, ulinzi shirikishi na serikali za mitaa katika maeneo ambayo sherehe hizo hufanyika, hawana budi kushiriki kudhibiti suala hilo. Uweke utaratibu kwamba watakaohusika kuruhusu watoto kuingia kwenye sherehe hizo, wakiwamo wamiliki wa kumbi, wachukuliwe hatua. Wamiliki wa kumbi watiliwe mkazo zaidi kuhusu jambo hilo na wanapokiuka wapewe kibano kikali kwa kufungiwa kufanya shughuli za kibiashara.

Tunasema hivyo kwa sababu katika sherehe za harusi na za kuwaaga mabinti kwenda kuanza maisha ya ndoa, kumekuwa na mambo mengi ambayo hayafai kwa watoto kama matumizi ya vileo.

Je, watoto wanajifunza nini wanapoyaona mambo hayo yakifanywa na wazazi? Wahenga wanasema mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Kwa mantiki hiyo, kuwashirikisha watoto katika matukio hayo ni kuwafundisha kutumia vileo na hali hiyo itawafanya kuanza kuiga kunywa pombe wangali wadogo.

Wakati ni sasa wa kuchukua hatua dhidi ya ukiukwaji huo wa sheria ya mtoto kwa kuwa kuendelea kuwapo kwa matendo hayo ni kuzidi kuwadhalilisha na kutweza utu wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

## Kandarasi za uzoaji taka mitaani wapewe wakazi wa maeneo hayo

**KUMEKUWA** na sitonfahamu ya utunzaji wa mazingira na ukusanyaji taka zinazozalishwa kwenye makazi kwa baadhi ya mitaa ya Jiji la Dar es Salaam.

Hali hiyo imesababisha kukithiri kwa uchafu wa mazingira katika maeneo mbalimbali, kutokana na changamoto za ukosefu wa vitendea kazi na magari.

Katika mitaa hiyo, kumekuwa na lundo la taka zilizokusanywa kwenye viroba pembezoni mwa mitaa, barabarani, vichochoroni na maeneo ya wazi kwa muda mrefu.

Takataka hizo pia hutupwa kwenye mitaro na kusababisha kero kwa wananchi kutokana na maji kusambaa barabarani mvua zinaponyesha na kutishia kuibuka kwa magonjwa ya milipuko.

Baadhi zinatupwa nyakati za usiku na nyingine kutelekezwa barabarani wakati wafanyakazi wa makampuni hayo kwa kushirikiana na wa serikali za mitaa wanapopita kukusanya takataka kwenye maeneo ya wakazi hao.

Magari hayo kila wiki hupita kwenye mitaa ya maeneo husika baada ya watendaji wa ofisi ya serikali za mitaa kupita wakitangaza kwa kutumia vipaza sauti kuwataka wananchi kutoa takataka na kulipa fedha ili kuyawezesha magari ya kampuni hizo kukusanya taka na kuzisafirisha hadi dampo zilipo.

Kiwango kikubwa cha taka hizo zinazozalishwa majumbani, zinajumuisha pampasi zilizotumika kuwasitiri watoto wadogo na wagonjwa wanapojisaidia haja ndogo na kubwa.

Pampasi hizo, ndizo zinazoongoza kwa kuzagaa mitaani, hali inayoonyesha kwamba ufumbuzi wa jinsi ya kuzitekeza haujapatikana katika jamii, licha ya matumizi yake kuwa makubwa. Kimsingi, ni elimu imekosekana kwa jamii.

Takataka nyingine zinazokuwa kwenye viroba hivyo, ni mabaki ya vyakula, vinyesi vilivyohifadhiwa kwenye mifuko na mikojo kwenye chupa za plastiki. Takataka kama hizo na nyingine, magurudumu ya magari, pia zimezagaa kwenye makazi ya watu na kugeuka kero na mazalia ya mbu na wadudu wengine.

Licha ya kuwapo kwa kampuni hizo za uzoaji taka katika maeneo hayo, changamoto kubwa inayojitokeza ni uhaba wa magari na nyingine ni maeneo mengine kutofikika kwa urahisi kutokana na ujenzi holela.

Kampuni hizo za uzoaji taka, nyingi zinapatikana baada ya kushinda kandarasi za uzoaji takataka katika halmashauri za maeneo husika na hiyo inaweza kuwa sababu ya kukosekana ufanisi katika kampeni ya kitaifa ya kuweka mazingira katika hali ya usafi.

Pamoja na jitihada hizo za halmashauri kwa kushirikiana na uongozi wa serikali za mitaa, ili kufanikisha kampeni hiyo ya usafi wa mazingira, kandarasi za uzoaji takataka, zingerudishwa kwenye mitaa ambako wananchi wangeshirikishwa.

Kushirikishwa wananchi katika mitaa yao kwa kiasi kikubwa kungeweza kurahisisha kampeni hiyo ya kusafisha mazingira kwenye makazi yao baada ya kuwekeana utaratibu maalum na kutungiana sheria kali. Wananchi hao watatekeleza majukumu hayo kwa kutumia vitendea kazi vya gharama nafuu kama mikokoteni badala ya magari na kupeleka taka eneo maalumu lililotengwa ambako zitasafirishwa na magari kwenda kutupwa dampo.

Vilevile, kwa kuwaachia jukumu hilo wananchi hao, mbali ya kuinua kipato katika kaya zao kwa kutoa ajira kwao na vijana, kutasaidia vizazi vyao kupata elimu ya namna ya kutunza mazingira, usafi na jinsi ya kukabiliana na magonjwa ya milipuko.

Hatua hiyo italeta hamasa kwa wananchi ya kuyapenda na kuyatunza mazingira yao kwa kuyaweka katika hali ya usafi wakati wote na si kusubiri viongozi wao kupita nyumba hadi nyumba kuwahimiza na kuitisha mikutano ya kujadili maendeleo.



Sehemu ya viongozi na watendaji wa sekta ya ardhi katika wilaya ya Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara, wakimsikiliza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (hayupo pichani), alipokwenda kufuatilia utekelezaji Maagizo ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# MSD yazidai bil. 20/- hospitali za rufani, vituo vya afya

**Na Pilly Kigome**

BOHARI Kuu ya Dawa Tanzania (MSD), inadai zaidi ya Sh. bilioni 20 hospitali za rufani na vituo vya afya Kanda ya Mashariki.

Madeni hayo yanatokana na kupatiwa dawa na vifaa tiba kutoka katika Bohari hiyo.

Hayo yalibainika jana jijini Dar es Salaam baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masulala ya Ukimwi, kufanya ziara katika Bohari Kuu Keko na ya Kanda ya Mashariki, iliyopo Mabibo.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, alisema moja ya changamoto inayowakabili ni madeni yanayokadiriwa kufikia kiasi hicho cha fedha baada ya vituo hivyo kupatiwa dawa na vifaa tiba kutoka katika Bohari hiyo.

Alisema MSD haiwezi kumnyima mteja dawa ama vifaa tiba anapokuwa na uhitaji kwakuwa ni huduma muhimu katika ustawi wa jamii na dawa zikiendelea kukaa muda mrefu zinaharibika kwa kuisha muda wa matumizi.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alikiri kuwapo kwa deni hilo kubwa ambalo Bohari hiyo inadai na tayari Rais Samia Suluhu Hassan alishaelekeza kuwa kila mtoa huduma ni lazima alipwe fedha zake ndani ya siku 60.

Mollel alisema amelipokea suala hilo na kulifanyia kazi kwa kuwa linahusisha taasisi zingine zilizo chini ya wizara yake.

"Tutahakikisha deni hilo linalipwa na kuwachagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya pia kusimamia na wawe na makadirio ya bajeti ya uagizaji dawa ili kusiwe na upungufu unaojitokeza," alisema.

Alisema lengo la ziara hiyo ni kuhakiki yatokanayo katika Bohari hiyo ikiwamo kujua mnyororo mzima wa uagizaji hadi kusambazwa dawa na vifaa tiba ikiwamo na kuboresha mifumo kutoka Bohari hiyo kwakuwa wana lengo la kwenda mbali zaidi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu Afya na Masuala ya Ukimwi, Stanslaus Nyongo, aliipongeza kwa kuridhishwa na utendaji wa Bohari hiyo wa kusambaza dawa na vifaa tiba katika hospitali za mikoa na taifa ikiwamo vituo vya afya.

Alibainisha kwa sasa MSD imeongeza tija na usambazaji wa dawa umeongezeka kufikia asilimia 95 hadi 99 katika hospitali za mkoa na usambazaji katika vituo vya afya na zahanati kutoka asilimia 13 na kufikia asilimia 64.

Alikiri deni ndiyo chanzo cha kamati kupitisha MSD waongezewe mtaji ili kuleta tija na kufanya kazi zao kwa ufanisi wa majukumu yake.

Pia, wapo katika mikakati ya kuboresha miundombinu kujenga maghala kwa kuwa sasa wanalipa pango linalofikia Shilingi bilioni mbili kwa mwaka kwa mwezi ni Sh. milioni 180 kwa Bohari ya Kanda ya Mashariki iliyopo Mabibo.

Meneja Kanda ya Mashariki MSD, Beata Kahema, alibainisha wanahudumia mikoa mitatu ikiwamo Morogoro, Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar na jumla ya vituo 966 kutoka halmashauri 23.

# Silaa ataka utatuzi migogoro ya ardhi haraka

**Na Munir Shemweta,** NANYUMBU

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amehimiza wakuu wa mikoa nchini kutekeleza maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

"Niwaombe wakuu wa mikoa yote nchini kuendelea kusimamia utekelezaji maagizo ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na migogoro ya vijiji 975," alisema.

Waziri Silaa alisema hayo juzi wakati akizungumza na uongozi wa Wilaya ya Nanyumbu, mkoani Mtwara akiwa kwenye ziara ya siku moja kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumzi ya ardhi katika vijiji 975.

Alisema, ameridhishwa na utekelezaji wa maamuzi hayo kwa Mkoa wa Mtwara kupitia Wilaya ya Nanyumbu na kwa mujibu wake wilaya hiyo imetekeleza maagizo hayo kwa asilimia mia moja.

Alisema, atahakikisha serikali inapotoa kauli lazima itekelezeke kwa kuwa ndiyo kazi aliyotumwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kuweka bayana kuwa, kazi aliyotumwa ataifanya mapema na kupeleka majibu ya mpango wa serikali kwa wananchi wa Nanyumbu ili kupunguza taharuki.

"Mimi naamini utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri utakamilika kwa haraka kwa sababu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ni maelekezo mahsusi ya Rais Samia, kuwa wizara ihakikishe jambo hili linafika mwisho," alisema Waziri Silaa.

Alisema, migogoro ya ardhi inahusisha watu na utatuzi wake unapocheleweshwa unaleta mgogoro mwingine mkubwa kuliko wa awali jambo alilolieleza utatuzi wake unaweza kuwa mgumu kwa sababu wa pili unaondoa imani ya wananchi kwa jambo lililoamuliwa na serikali kuwa linaweza kutekelezeka kwa haraka.

"Kwa kuwa kamati ilishaenda maeneo yote kasoro Peramiho, wajibu wangu ni kupita maeneo yote kwenda kuangalia utekelezaji maagizo ya Baraza la Mawaziri na nikiri tu utekelezaji wa maamuzi hayo kwa baadhi ya maeneo unasuasua," alisema.

Maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 yanatokana na timu iliyoundwa kuchunguza changamoto za uvamizi wa maeneo ya hifadhi ambayo iliwasilisha taarifa ya migogoro katika vijiji 366 na kuundwa Kamati ya Mawaziri wa Wizara za kisekta mwaka 2019, iliyokuja na mapendekezo ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975 huku vijiji 55 utatuzi wake ukisalia.

Wizara za kisekta zinazohusika katika utatuzi huo ni Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama mwenyekiti, Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, Kilimo, Maji, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), TAMISEMI na Wizara ya Ulinzi.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# Ridhiwani Kikwete awashukia maofisa utumishi uwajibikaji

**Na Lusungu Helela,** BUNDA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amewaagiza Maofisa Utumishi wa Halmashauri zote nchini kwenda kutembelea ofisi za watumishi katika kata na vijiji ili kutatua changamoto zao.

Pia, amepiga marufuku tabia ya baadhi ya Maofisa Utumishi kutoa vibali vya kusafiri kwa maofisa kwenda Dodoma Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kufuatilia masuala yao binafsi ya kiutumishi ilhali kazi hiyo ni ya maofisa utumishi hao.

Alisema watumishi hao hufika Dodoma kufuatilia kupandishwa madaraja, kubadilishiwa miundo na kada, kudai malimbikizo ya mshahara na kuonya vitendo hivyo vinawanyima fursa wananchi kuhudumiwa kutokana na maofisa hao kusafiri.

Kikwete alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, ikiwa ni siku yake ya tatu ya ziara anayoendelea kufanya mkoani Mara na kuwataka Maofisa Utumishi hao kuleta matumaini kwa watumishi wenzao.

"Acheni ile tabia ya kuonekana miungu watu, tatueni matatizo ya watumishi," alisisitiza.

Aliwakumbusha wajibu wao ni kutambua wateja wao namba moja na lazima wawape kipaumbele katika kutatua changamoto zao ili kupata matokeo makubwa.

"Katika ziara zenu mtakazojipangia za kutembelea vituo vya kazi hakikisheni mnatatua changamoto za watumishi wenu huku mkitumia nafasi hizo kwa kuwapatia taarifa za fursa mbalimbali za kiuchumi na za kujiendeleza kielimu zinazopatikana kwa sasa," alisema.

Aidha, alisema haipendezi kuona hata masuala madogo ya kiutumishi yanayowakabili watumishi wao yanasubiri hadi siku waziri au naibu waziri atoke Dodoma aje kuyatatua.

Aliwakumbusha utendaji kazi zao uwe wa kimkakati na sio kufanya kazi kwa mazoea

Alisema moja ya jukumu la msingi kwao ni kuhakikisha watumishi wanaowaongoza wanatatuliwa changamoto zinazowakabili hata ikibidi kufika Dodoma wasisite kwenda.

"Maafisa Utumishi hakikisheni mnajipangia ratiba ya kutembelea vituo vyenu zungumzeni na kusikiliza kero za watumishi, sitegemei nikija tena nisikie changamoto ndogondogo kutoka kwa watumishi wenu," alisisitiza.




Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, akisoma mabango ya ujumbe mbalimbali baada ya kuwasili katika Kituo cha ATFGM Masanga, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime akiwa kwenye ziara yake mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yakumbushwa kujengea wazee wasiojiweza makazi

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

SERIKALI kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeihimiza jamii nchini kukumbuka ujenzi wa makazi ya wazee wasiojiweza wakati huu wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, alisema hayo wakati akishiriki shughuli za maendeleo wilayani Tarime, mkoani Mara.

Akiwa kwenye ujenzi wa nyumba ya daktari wa zahanati ya Kijiji cha Soroneta, aliitaka jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo ili wawe na umiliki wa miradi hiyo waitunze ili idumu.

Mwanaidi alisema, Kampeni ya 'Amsha Ari' ni moja ya juhudi za serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 inayohimiza wananchi kujitolea wakati wa shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao.

"Mimi nimekuja hapa kuamsha ari ya wananchi kujenga makazi bora na pia kusaidia watu wengi kuwa na makazi bora hasa wazee wasio na uwezo," alisisitiza Mwanaidi.

Diwani wa Kata ya Nyarelo, Japheth Marwa, alisema wananchi wa kata hiyo wana moyo na ari ya kujitolea katika shughuli za maendeleo na wataendelea kujitoa ili kufanikisha miradi mbalimbali ya huduma za jamii iweze kuwasaidia kuondokana na changamoto zinazowakabili.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kijiji cha Soroneta, Kata ya Nyarelo, Dk. Richard Kitende, aliishukuru serikali kwa kuunga mkono juhudi za wananchi kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuwa inasaidia kuwapa moyo wa kujitoa na kusaidia upatikanaji wa huduma muhimu karibu na maeneo yao.

Akizungumzia hatua hiyo, Mbunge wa Tarime Vijijini Mwita Waitara, alisema ni jambo jema viongozi kuonesha mfano kwenye masuala ya maendeleo na jamii kwa kuwa itasaidia kuwa na moyo na mwamko kwa wananchi kuchangia katika shughuli za maendeleo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Janeth Michael, alisema mradi huo umeshirikisha wananchi kwa shughuli za kuchimba msingi, kusomba mawe na kujenga boma na gharama zote za nguvu ya wananchi ni Sh. milioni 8.1 huku wakiungwa mkono na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime iliyotoa Sh. milioni 20.

# Tanzania yashinda kuwa mwenyeji mkutano wafuga nyuki duniani 2027

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imeshinda nafasi ya kuwa mwenyeji wa Kongresi ya 50 ya Shirikisho la Vyama vya Wafuga Nyuki Duniani (APIMONDIA), inayotarajiwa kufanyika Septemba 20 hadi 25, 2027, jijini Arusha baada ya kuzishinda nchi nne zilizokuwa zikishindanishwa ikiwamo China, Togo na Umoja wa nchi za Falme za Kiarabu (UAE).

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angela Kairuki, alisema katika hatua ya fainali iliyoshindanisha nchi mbili, Tanzania ilishinda kwa kupata kura 65 dhidi ya 38 za UAE, zilizopigwa na wajumbe wa nchi wanachama wa shirikisho hilo katika mkutano mkuu wa 48 wa Shirikisho hilo uliofanyika Septemba 8, mwaka huu, UAE.

"Natoa shukrani kwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye aliridhia Tanzania kushiriki na kuwania nafasi hiyo. Ushindi huo unaifanya nchi yetu kuwa ya pili kwa Bara la Afrika na kupewa heshima hiyo kubwa ya kuandaa Kongresi hiyo tangu kuanzishwa kwake miaka 130 iliyopita, nchi nyingine ambayo iliwahi kupata nafasi hiyo ni Afrika Kusini mwaka 2001," alisema Kairuki.

"Ushindi huu ni ushahidi tosha kwamba serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo mipango yake ya kuhakikisha sekta ya maliasili inazidi kuimarika ili kuendelea kutunza rasilimali za nchi na kuyafanya mazao yatokanayo na maliasili na nyuki kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi, kuongezea wananchi kipato na kutengeneza fursa zinatotokana na bidhaa hiyo."

Alisema zaidi wa washiriki 6,000 wanatarajia kuhudhuria kwenye kongresi hiyo kutoka mataifa mbalimbali duniani.

"Kwa hiyo kupitia mkutano huo, Tanzania itapata manufaa mengi ikiwamo kuendelea kuchochea ukuaji wa sekta ya nyuki na uhifadhi, kuongeza mchango wa zao hilo katika pato la taifa hususani kupitia biashara na uwekezaji, viwanda na teknolojia na kuchochea shughuli za uchumi nchini.

Alisema wameunda kamati ya maandalizi ambayo itafanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa sekta hiyo ili kuhakikisha mkutano huo unafanyika kwa ufanisi na kuacha alama kwa wote watakaohudhuria.

Aliwataka wafanyabiashara na wadau mbalimbali kujiandaa kuchangamkia fursa mbalimbali zitakazopatikana kutokana na mkutano huo.

Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alisema miongoni mwa mambo yaliyochangia Tanzania kushinda nafasi hiyo ni pamoja na utayari kwenye miundombinu yake katika uzalishaji kwenye sekta hiyo.

Alisema Tanzania inashika nafasi ya 14 duniani kwa uzalishaji wa mazao yatokanayo na nyuki wakati katika Bara la Afrika inashika nafasi ya pili.



Mratibu wa Tiba Utalii wa Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita (katikati), Mganga Mfawidhi wa Hospital ya Rufani ya Mkoa wa Arusha Mount Meru, Dk. Alex Ernest (kushoto) na Dk. Liggyle Vumilia kutoka wizara hiyo, wakikata keki kuzindua mafunzo na mkutano wa kwanza na wadau mbalimbali uliojadili masuala ya Tiba utalii yaliyoandaliwa na hospitali hiyo, jijini Arusha juzi, kwa lengo la kukuza uelewa wa washika dau juu ya ajenda ya Tiba utalii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko: Bado kuna ulegevu katika sera, sheria za ardhi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri Mkuu, Dotto Biteko, amesema pamoja na kuwa na ubora wa sera na sheria za ardhi nchini, bado kuna ulegevu, hivyo kunahitajika kujifunza kwa wengine wenye uzoefu zaidi.

Amesema licha ya ubora wa sheria zilizoko za ardhi, bado maboresho ni muhimu kufanyika ili kwenda sambamba na kasi kubwa ya ukuaji wa teknolojia.

Aliyasema hayo jijini hapa kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akifungua Kongamano la Nne la Taasisi za Ardhi Afrika linaloongozwa na ajenda ya upatikanaji wa hakimiliki za ardhi.

"Sisi Tanzania pamoja na ubora wa sera na sheria zetu lakini bado kuna sehemu tunalegalega na sisi tunahitaji kujifunza kwa wengine wenye uzoefu zaidi yetu na sisi tunahitaji kufundisha wengine, hivyo kupitia uzoefu tutakaobadilishana hapa naamini mtachukua hatua ya kufanya maboresho mtakayoona yanahitajika,"alisema.

Aidha, alisema baadhi ya mafanikio waliyoyafikia kama nchi, yametokana na uhusiano na washirika mbalimbali wa maendeleo ikiwemo Benki ya Dunia (WB), kwa sababu ya uhusiano mzuri na jitihada za kutafuta fedha.

"Tanzania imefanikiwa kusaini mkataba na Benki ya Dunia yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 150 kwa ajili ya kuboresha usalama wa milki za ardhi. Itakuwa na lengo la kutoa hati za haki milki milioni 2.5 ifikapo mwaka 2026, ikiwa ni mradi wa kwanza kupata fedha nyingi katika sekta ya ardhi kutoka Benki ya Dunia katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara,"alisema.

Alisema pamoja na majadiliano ya kitaaluma watakayoyafanya kwa siku tatu watakazokuwa hapo, aliwaagiza kujadili namna ya kupata rasilimali fedha, kwa ajili ya kuendeleza sekta ya ardhi katika nchi za Afrika.

Kadhalika, aliwaagiza Watanzania kila mwenye kipande cha ardhi hata kama ni kidogo kuhakikisha anakuwa na hati miliki kwa faida ya vizazi vijavyo.

Pia, akiwataka kushikamana, kuisaidia sekta ya ardhi Afrika kuwa na sera na miundo mizuri ya usimamizi na utawala wa ardhi na kuinua uchumi wa nchi wanachama, kuondoa migogoro.

Vilevile, alisema iwapo kila mmoja wao kwa nafasi yake akitimiza wajibu wake kikamilifu, anaamini watachangia kuleta matokeo chanya katika sekta ya ardhi kwa nchi wanachama.

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Slaa, alisema zipo changamoto nyingi za ardhi zinazowakabili nchi za Afrika kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi Zanzibar, Juma Makungu Juma, alisema Mapinduzi ya Zanzibar yalitokana na ardhi na ndiyo maana Zanzibar inalichukulia suala la ardhi kwa umuhimu mkubwa.

Alisema: "Bila ardhi hakuna maisha. Nawaalika wawekezaji karibuni Zanzibar na ikipendeza kama kongamano lijalo litafanyika Tanzania karibuni mfanye Zanzibar"

Mratibu wa Shirika la Resource and Rights Initiative (RRI), Dk. Solange Bandiaky, alisema Tanzania ni nchi ya mfano Afrika kwa kuwa na mpangilio bora wa matumizi ya ardhi.

# Waziri asema wanaandaa sera zinazokidhi mabadiliko kiteknoloji

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Mathew Kundo, amesema Tanzania inatarajia kuweka sera zitakazoendana na mabadiliko ya teknolojia katika uendelezaji wa miji maridadi duniani.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Shirika la Mawasiliano la Kimataifa la (ITU), uliowakutanisha wataalamu wa teknolojia na mawasiliano kutoka ndani na nje ya nchi.

Mhandisi Kundo alisema uchumi wa kidijitali ndio utakaowezesha kuendanana na miji ya kisasa duniani.

Alisema sera hizo zitawezesha Tanzania kujipanga zaidi na kuweka sera zinazoendana na mabadiliko ya teknolojia hiyo, kwani dunia kwa sasa inakwenda kwenye uchumi wa dijitali wa kupata huduma yoyote kwa kutumia kadi bila kuwa na fedha taslimu.

Aidha, alisema miji maridadi itabadilisha teknolojia kuwa za kisasa zaidi, katika ukusanyaji taka, ubora wa miundombinu ikiwemo biashara inayokua kwa kasi, sanjari na utoaji huduma bora za mawasiliano na nyinginezo.

"Ili kufikia hatua hii ni lazima sasa tuwe na sera nzuri, ambazo sasa tunazifanyia maboresho zaidi, ili Tanzania iendane na kasi ya teknolojia, hasa katika upangaji wa miji maridadi,"alisema

Mhandisi Kundo alisema washiriki wa mkutano huo wanajadili maendeleo na changamoto zinazohusiana na teknolojia za mawasiliano na habari, katika ngazi ya kimataifa ikiwemo kikundi cha utafiti cha ITU-T.

Alisema vikao hivyo vinawakutanisha wataalamu na wabunifu kutoka duniani, kujadili mweleko wa IoT na jinsi teknolojia hiyo inavyoweza kubadilisha maisha na namna tunavyoishi na kufanya kazi katika miji na jamii.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk.Jabir Bakari, alisema mkutano huo utachangia kuimarisha uchumi wa kidijitali nchini na fursa ya kujifunza kutoka kwa nchi nyingine na kushirikiana ujuzi wake, katika miji maridadi kutokana na wataalamu na wabunifu nchini kupata nafasi ya kujadiliana na wenzao kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Pamoja na majadiliano kuhusu IoT na miji smart, mkutano pia unajumuisha masuala mengine muhimu kama usalama wa mifumo ya IoT na faragha, viwango vya teknolojia hizo na faida za kiuchumi zinazotokana na maendeleo haya.

Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe alisema miji maridadi inaendana na ukuaji wa kasi za utoaji huduma za maendeleo, ikiwemo ukuaji wa kasi ya teknolojia za mawasiliano kwenye TEHAMA katika utoaji huduma bora kwa wananchi kama ilivyo kwa Jiji la Dodoma ambalo ni miongoni mwa Jiji linalotengenezwa na kukua kwa kasi.

# Wahitimu vyuo vikuu wapewa siri kufanikiwa kimaisha

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

VIJANA wanaohitimu vyuo vikuu wametakiwa kuachana na utegemezi wa ajira za serikali, badala yake wajiunge na mafunzo ya ubaharia na uhandisi zenye watalamu wachache duniani.

Ushauri huo umetolewa jana mkoani hapa na mmoja wa wataalamu wa masuala ya ufuatiliaji na tathimini kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulamavu, James Mallya, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kongamano la pili la kitaifa la wiki ya ufuatiliaji na tathimini.


Alisema kwa Tanzania vijana hawana sababu ya kukosa mafunzo hayo kwa sababu tayari kuna Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) ambacho kinatoa kozi hizo na kusaidia vijana wengi wanaohitimu kuajiriwa kwenye vyombo vya majini ndani na nje ya nchi, sababu ya uchache wa wataalamu hao.

Alisema kozi hiyo inafundisha kijana kupata ujuzi hata wa uokoaji majini, hivyo akiwa na ujuzi huo hawezi kukosa kazi ya kufanya hata kwa kujiajiri pamoja na kupata fursa ya kwenda nje ya nchi kupata uzoefu zaidi na kuachana na utegemezi wa serikali au wazazi.

Naye Makamu Mkuu wa DMI (Idara ya Mipango, Fedha na Utawala), Dk.Lucas Mwisila, alisema chuo hicho kinazalisha wataalamu wenye uwezo wa kufanya ufuatiliaji, tathimini, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuleta matokeo chanya kazini.

"Lengo la kutoa kozi zenye wataalamu wa aina hii ili kuwezesha jamii kupata huduma zenye tija kwao na taifa, sababu pale unapofanya kitu bila kufanya ufuatiliaji na tathimini huwezi jua kama ni kizuri au la na unapofahamu kasoro zake zinarekebishwa mapema na kutoa huduma zinazokidhi vigezo vinavyohitajika katika jamii,"alisema

Pia, alisema moja ya faida za wataalamu kuzingatia ufuatiliaji na kufanya tathimini, husaidia mazao yanayopatikana ndani ya bahari, kama mwani, mafuta, umeme au samaki, yote yafike katika masoko kwa wakati.





# Simbachawene aagiza ma-RC, ma-DC kusimamia uwajibikaji

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewaagiza viongozi wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanasimamia uwajibikaji kwa watumishi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo jana akiwa katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita baada ya kuwasili mkoani hapa kwa ajili ya ziara ya kikazi ya siku tatu yenye lengo la kukagua utekelezaji wa majukumu ya viongozi na watumishi wa umma.

Alisema katika maeneo mengi yakiwemo taasisi za serikali ikiwemo hospitali, vituo vya polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kumekuwa na uzorotaji katika utolewaji wa huduma kwa wananchi.

Alisema kumekuwa na ucheleweshaji wa kupata huduma kwenye maeneo hayo hali inayoipotezea uaminifu serikali kwa wananchi.

"Wakuu wa mikoa na wilaya nchini hakikisheni changamoto ya uzorotaji wa utoaji huduma kwa wananchi inakoma kwenye maeneo yenu, Rais Samia Suluhu Hassan, anahitaji kuona huduma stahiki za kijamii zikitolewa ipasavyo," alisema Simbachawene.

Akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Geita kuhusu mchakato wa watumishi kuhama kwenye vituo vyao vya kazi, aliwataka watendaji kusimamia sheria kutokana na uwepo wa baadhi ya watumishi wanaomba kuhama kutoka vijijini kwenda maeneo ya mjini na kuacha nafasi zikiwa wazi.

Alisema hali hiyo inasababisha uhaba wa watumishi maeneo ya vijijini.

Kadhalika, aliitaka mifuko ya huduma kwa watumishi nchini ikiwemo PSSF, kufuatilia taarifa za waajiriwa kwa waajiri wao badala ya waajiriwa wao kufanya ufuatiliaji.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela alisema maagizo hayo wameyapokea huku akiahidi kuyafanyia kazi kama inavyo stahili.

Simbachawene yupo mkoani Geita kwa ziara ya kikazi ya siku tatu ambako atatembelea na kukagua miradi ya maendeleo na kuongea na watumishi halmashauri kwenye Wilaya za Geita, Chato na Bukombe.

# Wadaiwa kuvamia Uwanja wa Ndege, wajenga nyumba

**Na Remmy Moka, SAUT**

NYUMBA zipatazo 800 za wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, zinadaiwa kujengwa katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Mwanza hali inayosababisha migogoro ya mara kwa mara kati ya wamiliki wa nyumba hizo na uongozi wa uwanja huo.

Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni wa tatu kwa ukubwa nchini kati ya viwanja 52, kwa sasa umekumbwa na uvamizi huo ambao unaathiri usalama wa wakazi wa maeneo hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, Meneja wa uwanja huo, Mussa Mcholla, alisema uvamizi huo unaondoa usalama wa uwanja na Jeshi la Anga.

Hivyo, aliiomba serikali kuwaondoa wananchi hao waliovamia, kuyaacha maeneo hayo kwa ajili ya maendeleo ya uwanja, usalama wa taifa pamoja na usalama wao wenyewe.

Alisema wananchi kujenga karibu na uwanja wa ndege kuna athari zinazoweza kujitokeza endapo ikitokea hitilafu

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amosi Makalla, amesema kama suala la mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na serikali eneo la uwanja hautaondoka ndoto za uwanja huo kuwa wa kimataifa inakufa.

Alisema pia usalama wa nchi, wananchi na jeshi hauotokuwa wa uhakika, pia marubani wanaohitaji mazoezi katika uwanja huo hawatoweza kufanya.

Aidha, alieleza kuwa serikali kupitia Baraza la Ardhi la Wizara imeagiza kuwaeleza wananchi waliovamia eneo hilo kuondoka ifikapo Desemba mwaka huu, kwamba asiwepo mwananchi yeyote atakayebaki katika eneo hilo.

Alisema Uwanja wa Ndege wa Mwanza ukiwa wa kimataifa ni fursa ya kimafanikio kwa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa itafunguka, huku akitoa maelekezo kuona mbinu madhubuti za kujenga uwanja huo kwa hadhi ya kimataifa na hoteli za kisasa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilemela, Yusuphu Bujiku, ameiomba serikali itumie busara kuwaondoa wananchi hao katika uwanja wa ndege ili kuepusha migogoro hiyo.

Katika hatua nyingine Makalla aliweka jiwe la msingi katika Shule ya Msingi Buteja iliyopo wilayani Ilemela, Kata ya Kahama iliyojengwa kwa mradi wa 'boost', na kuwaomba walimu na wazazi kuhakikisha wanatokomeza tatizo la utoro kwa wanafunzi.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange (kushoto), wakati wakishiriki kwenye usafi mazingira ya mitaa ya mji wa Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mwanafunzi abuni mfumo kuwasha, kuzima taa kwa simu

**Na Jenesta Jasson,** BUKOBA

MWANAFUNZI anayesomea fani ya usanifu umeme katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) mkoani Kagera, Medisedeck Masalu (21), amebuni mfumo wa kuzima na kuwasha umeme ndani na nje ya nyumba kwa kutumia ujumbe wa simu.

Akionyesha ujuzi huo mbele ya Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni, Afya na Michezo chuoni hapo alisema mfumo huo unaweza kuwasha taa kwa umbali wowote kwa kutumia ujumbe kwenye simu ambayo imeunganishwa na mfumo huo.

Aidha, aliiomba serikali kuwasaidia vijana wanaosoma ujuzi mbalimbali katika vyuo vya ufundi, ili waweze kufanya ubunifu zaidi kwa ajili ya maendeleo.

Mkufuzi wa chuo hicho, Yohana Mwachali, alisema kuwa wanafunzi wa chuo hicho wanaoneka kuwa na ubunifu mbalimbali lakini wamekuwa wakikosa kuendelezwa.

Mbunge Thea Ntara, alieleza kuwa katika kutengeneza Tanzania ya viwanda, serikali inahitaji ubunifu, hivyo aliishauri serikali kuwatambua vijana wenye ubunifu na kuwaunga mkono ili waweze kuonesha kazi zao na kufikia malengo ya taifa.

Naye Mwenyekiti wa kamati hiyo, Khusina Sekiboko, alipongeza vijana hao wenye ubunifu mbalimbali na kuwashauri kutokusubiri ajira serikalini, bali kile walichowezeshwa katika mafunzo yao kukitumia ipasavyo kuhakikisha wanatimiza ndoto zao.

Mkurugenzi wa chuo hicho, Antony Kasole, licha ya kuishukuru serikali aliahidi kusimamia katika ushauri wa kamati hiyo juu ya kuwaandaa vyema vijana katika kujitengemea kwenye soko la kujiajiri ili kufikia dhamira ya Tanzania ya viwanda kwa kutengeneza vijana wenye ujuzi mkubwa.




Ukurasa 13

Anayetaka kubebwa kama jeneza mwacheni abebwe!'



**SIKU YA TAIFA YA BIMA**
**Msimamizi Mkuu wa fani aorodhesha mafanikio, apiga debe wakati umetimu kuwapo Bima Kilimo**

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 15, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

SAFARI YA 'KILIMO CHA KUFA NA KUPONA'

# Sekta kilimo inavyobaki mtaji Taifa tangu zama za Mwalimu hadi Samia

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupatikana Uhuru wa nchi mipango ya maendeleo na hususani kuanzia mwaka 1964, ilikuwa na malengo maalum kuboresha maisha ya Mtanzania mmoja mmoja, pia taifa kwa ujumla.

Ni bahati mbaya, wakati huo takribani sekta zote zilikuwa chini kimaendeleo, maana nchi ilikiwa chini ya utawala wa kikoloni na mfumo wa uchumi na maendeleo ulidumu kunufaisha watawala.

Hivyo, mageuzi ya Uhuru wa nchi mbalimbali na kukuza kiwango katika sekta za maendeleo, pia yalilenga kukuza huduma katika sekta za maendeleo kama vile elimu na afya kwa umma.

Katika uzalishaji, nchi ikabaki mitaji ya umma kukiwa na maendeleo duni ya uzalishaji viwandani ambavyo havikuwapo. Nchi ilikuwa chanzo cha rasilimali kwa wageni kama vile malighafi na madini.

Hadi uhuru na miaka michache baadaye, mwaka 1964 ukaandaliwa Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo 1964 -1969. Mfumo wa uchumi ulioachwa na ukoloni ulikuwa na sura ya "tunazalisha tusichotumia na kutumia tusichozalisha."

Malighafi kutoka kwa mwajiri mkuu wa umma wakati huo hadi sasa, sekta ya kilimo yalisafirishwa kwenda nje ya nchi na bidhaa zake zinaingizwa nchini kutumiwa kama vile nguo.

Hapo ndipo sauti ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Uchumi ikachukua nafasi yake, kuvunja mpaka wa kasoro iliyokuwapo "tunatumia tulichozalisha na kuzalisha tunachotumia..."



Wakulima wa Pamba Kijiji cha Mangungu, Kata ya Bukoko wilayani Igunga, wakiwajibika shambani. **PICHA: MTANDAO.**

Zao mojawapo ndani ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo huo wa 1964 hadi 1969, kukaibuka utitiri na kukomaa kwa viwanda vya nguo nchini, kama vile Sunguratex na Urafiki vya Dar es Salaam, Tabotex (Tabora) na Mutex (Musoma), kutumia pamba ya mashamba nchini.

Daima muda wote tangu zama hizo hadi sasa, kuanzia kiitikadi, kisera na mipango mikuu ya kiuchumi, kilimo kimebaki kuwa mhimili nyeti katika uchumi wa nchi na haujawahi kugota kuajiri chini ya theluthi mbili ya Watanzania wote.

Hata baada ya miaka 10 ya uhuru wa nchi kufika, ambao Rais Juluus Nyerere, aliupokea kwa tabasamu ya mafanikio kimaendeleo nchini akiorodhesha mengi, kukapitishwa maazimio makuu ya kitaifa ndani ya miaka michache, kutoka kwenye chama cha tawala TANU, ikiwamo Azimio la Iringa mwaka 1972, 'Siasa ni Kilimo.'

**HALI ILIVYO SASA**

Leo hii ikiwa ni awamu ya Sita ya Uongozi wa nchi, Rais Dk. Samia, katika kauli yake wiki hii akiwa na wanasiasa, anawekeza falsafa na utekelezaji katika mema taifa imeyarithi kwa viongozi waasisi, tofauti inaegemea kwenda na mabadiliko ya wakati.

Ishara yake inajikita katika yaliyoamuliwa katikia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 1964, daima yameendelea kuchukua sura katika kilimo kama alivyochukua hatua mwasisi Rais Nyerere, ikiwamo na awamu zingine za miaka mitano, 1969 hadi 1974 na mwisho baada ya hapo.

Tofauti ya sasa inashuhudiwa katika maboresho ya mifumo, huku mwanzoni baada ya Uhuru ilijikita katika msingi wa kilimo bora na wakulima kujengewa mazingira ya tija ngazi ya msingi, kusambaziwa 'mabwana shamba' wakiwapa elimu na huduma za kilimo bora.

Hapo kukashudiwa hatua zaidi katika Mpango wa Pili, maboresho yakianza kupatikana trekta shambani, mkakati wa 'Kilimo cha Kufa na Kupona' na zikiguswa vijiji na vijiji vya ujamaa, vilivyokuwa na operesheni maalum mwaka 1974, zikisaidia na vivutio vya utafiti wa kilimo, sasa maarufu kwa jina la TARI.

Kilichoko sasa Awamu ya Sita Tanzania chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, umuhimu wa kilimo uko palepale. Kinazoshuhudiwa ni sekta hiyo kukidhi mahitaji katika sera na uchumi wa leo.

Kilimo kinaendelea kuimarishwa kuwa mzalishaji mkuu wa chakula na malighafi, huku ikipandishwa daraja kumudu mahitaji ya kisasa na kiteknolojia, huku ikidumu kuwa mwajiri mkuu,theluthi mbili ya Watanzania, ikiingiza robo ya pato la taifa sasa.

Mambo yanayowekewa mkazo sasa, yana sura zote kuendeleza yale ya mwaka 1964 katika sekta kilimo, tofauti ya anachojikita nacho Rais Dk. Samia na watangulizi wote wa awamu nne baada ya Mwalimu Nyerere, ni mabadiliko ya wakati akihudumia mwelekeo wa sasa, kuanzia uzalishaji, masoko na thamani ya mazao na namna inavyokidhi mipango uchumi iliyoko.

Mosi, kilimo kimedumu katika 'Uti wa Mgongo wa Taifa'. Taasisi ya Utafiti za Kilimo (TARI), inabaki nyenzo ya kihistoria kusimamia kitaalamu, kutafiti na kufanya ubunifu katika kilimo bora, kama vile kuvumbua mbegu bora na kukabili magonjwa ya kilimo,), kazi inasonga kwa kasi kukishuhudiwa mageuzi ya tija.

Juhudi hizo za TARI kwa karibu inadumu hadi sasa kupata ushirika jirani wa mkongwe, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), ambacho mwanzo wake kilikuwa Kitivo

Inaendelea Uk 12

**FEDHA**

## SIKU YA TAIFA YA BIMA

# Msimamizi Mkuu wa fani aorodhesha mafanikio, apiga debe wakati umetimu kuwapo Bima Kilimo

**Na Restuta James**

LEO dunia inaadhimisha Siku ya Bima, ikiwa ni moja ya tukio la kuongeza uelewa wa sera na umuhimu wa bidhaa za bima kwa ajili ya maisha ya kila siku ikiwamo 'bahati mbaya' zinazowakuta watu kila kukicha.

Umuhimu wa bima unatokana na uhalisia kwamba hakuna mtu anayetamani kuugua, kupata ajali, kuumia akiwa kazini, kupoteza maisha au mali ambayo ameichuma kwa jasho.

Kwa tafsiri rahisi ni kwamba faida ya bima ni kumhakikishia mtu matibabu pale anapopatwa na ugonjwa, faraja anapopata ajali, kifo, janga la moto kwenye nyumba na hasara ya mazao au mifugo inapotokea.

Akizungumzia kuhusu siku hiyo muhimu, Kamishna wa Bima wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, anasema faida ya mtu kuwa na huduma ya bima ni kujikinga na majanga au hasara anayoweza kuipata pale anapopata tatizo.

"Bima ni kinga kwa ajili ya mali, afya, majanga ya kiuchumi na kijamii. Ni sekta inayotoa kinga dhidi ya mali, maisha na afya," anasema.

Anasema kuna bima za kawaida ambazo ni magari na mali, maisha inayotoa pensheni na mafao mengine kama inavyokubaliwa, afya na takafuli ambayo inazingatia misingi ya dini ya Kiislamu.

Kamishna Saqware anasema faida za bima ni kuondoa umasikini na kuinua kipato hasa pale mtu anapopatwa na janga akieleza kuwa kila mtu anapaswa kuwa na bima ili kujilinda na kuwakinga wale anaowapenda.

"Tumefanikiwa kutoa leseni 1,300 hadi Septemba 2023, kumekuwa na ongezeko la asilimia 13... tumesajili watoa huduma tisa wa dijitali (digital insurance platform)," anasema.

Anahimiza kuwa, TIRA imeshatoa miongozo ya namna bora ya kuendesha sekta ya bima, ukiwamo wa usimamizi na ubakizaji wa bima na bima mtawanyo, uendeshaji na usimamizi wa gereji zinazohudumia sekta ya bima, usajili wa bima za fya.

"Kwa mfano tunataka tusajili gereji zinazotoa huduma za bima ili chombo cha moto cha mteja mwenye bima anapopata ajali atengenezewe gari yake kwa ubora unaotakiwa," anasema.

Anasema, mwongozo huo unaweka ukomo wa muda wa chombo kutengenezwa hadi siku 30 na kwamba inatoa mwanya kwa watoa huduma kushindana na kufanyakazi kwa ubora unaostahili.

Anasema, kwa sasa TIRA ina majukumu manne ya kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma, kuandaa miongozo na taratibu za bima nchini, kulinda wanufaika au wateja wa bima, kuishauri serikali kuhusu masuala yote ya kibima.

"Tumetekeleza vizuri masuala yote yaliyopo kwenye sheria kwa kipindi chote toka kuundwa kwa mamlaka," anasema.

Kihistoria nchini, baada ya historia ya nchi kuingia katika mfumo wa chama kimoja, miaka michache baada ya uhuru, huduma hiyo imekuwa ikiendeshwa na Shirika la Bima la Taifa (NIC), mbalo linadumu hadi sasa likiwa shirika la umma.

Vilevile, serikali ikajijengea msingi wa kupata wataaluma wa bima, kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), kilichoanzishwa mwaka 1972, kama ilivyo kwa wataaluma katika stadi za benki, na hifadhi ya jamii.



Magari yaliyopata ajali. Tathmini ya fidia yake, hurejea katika mashirika ya bima, ambayo umma unasisitiziwa kujiunga na huduma zake. **PICHA: MAKTABA.**

### GEREJI NA BIMA

Dk. Saqware anasema gereji zinazohudumia wateja wa bima, zinapaswa kumhakikishia muda atakaopata gari yake na ubora wa vifaa (spare parts), vitakavyofungwa kwenye chombo chake.

"Baada ya kujua wateja wetu wanahangaika, hawapati huduma inayolingana na thamani ya fedha yao, tukawaambia watu wa gereji kwamba lazima tuwasajili," anasema.

Anasema mwongozo wa TIRA wa Mei mwaka huu, unatoa nafasi kwa wahitimu wa kozi ya bima kusajiliwa na kampuni ya bima kuuza bidhaa za sekta hiyo bila ya kuwa na kampuni.

Mbali ya nafasi hiyo, anasema sekta hiyo imeingia kwenye uwanja wa kidijitali ambako tayari wamesajili bima mtandao tisa.

Anasema, mteja wa bima anaweza kukata bima mtandaoni na kufurahia huduma bila ya kulazimika kutembea na fedha taslimu.

"Tumesajili kampuni mbili za bima zinazozingatia misingi ya dini ya Kiislamu pamoja na washauri wa bima wanaouza bima hii ya takaful pekee," anasema.

Akizungumzia malipo kwa wanufaika wa bima, anasema wameshatoa mwongozo wa muda wa kulipwa madai pale mteja anapowasilisha madai pindi anapopatwa na janga.

"Tuna mwongozo wa kima cha chini cha kumlipa mtu anayepatwa na janga kama kugongwa na gari yenye bima kuna vigezo vimewekwa ili kuhakikisha mtu anayepata ajali analipwa stahiki zake na bima," anasema.

Anafafanua kuwa, mwongozo huo pia umeweka ukomo wa muda wa kulipa madai hayo kwa mtu aliyepata ajali.

### BIMA MPYA

Anasema TIRA imeishauri serikali kuanzisha Bima ya Kilimo, ili kuwaepusha wakulima na umasikini pale linapotokea janga la ukame, mafuriko au wadudu waharibifu kwa kupata fidia.

Kamishna anasema, lengo lililoko ni kuwafikia wakulima 10,000 ndani ya miaka mitano ijayo, ili kuwaondolea msongo wa mawazo pindi mazao au mifugo inapokutwa na tatizo.

Pia, anasema wameishauri serikali namna bora ya kushiriki uchumi wa mafuta na gesi kwa kuweka bima kwenye sekta hiyo ndogo.

"Tumeishauri pia serikali ikatie bima magari yake yote. Zanzibar imefanya hivyo na tunaendelea na mazungumzo na Serikali ya Jamhuri kuhakikisha inafanya hivyo," anasema Dk. Saqware.



Kamishna wa Bima wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware. **PICHA: RESTITUTA JAMES.**

Vilevile anataja eneo la bima limeshatoa ajira zaidi ya 4,500 pamoja na kuongeza mapato ya serikali kwa kulipa kodi.

Anasema hadi sasa, kuna mwitikio mkubwa wa watu kutaka kuzijua bidhaa za bima japokuwa kasi ya kupata taarifa kutoka kwa wadau au kampuni zinazotoa huduma hiyo ni ndogo.

### SURA YA MAGUMU

Penye mafanikio, hapakosi changamoto! Dk. Saqware anasema sekta ya bima inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo kutokuwapo kwa sera ya taifa inayosimamia sekta hiyo pamoja na wataalamu wa bima kutokuwa na bodi yao inayowasimamia.

Anasema, uwapo wa sera na bodi ya wataalamu, itawawajibisha zaidi wataalamu na sekta nyingine kuhakikisha kwamba bima inakuwa na viwango bora vinavyostahiki.

Dk. Saqware anasema elimu ya bima kwa jamii bado ni changamoto, kwani wananchi wengi hawajui umuhimu na faida za bidhaa hizo.

"Jambo la kusikitisha ni kwamba, mtu anajenga nyumba nzuri labda ya Sh. milioni 100, lakini haikatii bima. Bima rahisi zaidi ni ya nyumba na kwa yenye thamani hiyo bima yake kwa mwaka ni Sh. 75,000 ," anasema.

### DONDOO MUHIMU

Kwa mujibu wa Dk. Saqware kuna aina kadhaa za bima zikiwamo ya afya kwa ajili ya matibabu na vipimo, mazao na mifugo kwa ajili ya majanga ya kiuchumi, ajali kwa ajili ya kukinga nyumba na magari, maisha kwa ajili ya pesheni au fidia ya kifo kwa wanufaika wa mteja na ya tafakul inayozingatia misingi na sheria za dini ya Kiislamu.

Dk. Saqware anasema bima ya maisha ni uwekezaji na kinga kwa ajili ya maisha ya baadae kwa kuwa ni ya muda mrefu kuanzia miaka mitano na kuendelea.

## SEKTA KILIMO INAVYOBAKI MTAJI TAIFA TANGU ZAMA ZA MWALIMU HADI SAMIA

**INATOKA UK 11**

cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ni aina ya juhudi za kiserikali, zinaoendana na maboresho na ufuatiliaji wa karibu wa wizara dada, Mifugo, ambayo Rais Dk. Samia anaikagua 'kichwani hadi unyayoni' hata katika kilele cha sherehe za Nanenane mwaka huu akatamka 'sasa ninaridhika'.

Msamiati 'kilimo ni uti wa mgongo' unashuhudiwa kwa vitendo katika miaka mitatu iliyopita, imekuwa wizara inayopendekwa zaidi kuongezewa maradufu, sasa malengo ni kukifanya kuwa cha kisasa, sicho cha kutegemea mvua pekee.

Hamasa hiyo inaendana na kuboresha uchumi wa nchi, kuanzia chakula, malighafi na mapato ya mazao, hata ngazi ya soko la kimataifa na fedha za kigeni.

Mradi wa mfano kuajiri umma zaidi, hasa kada ya vijana wasomi wahitimu wa chuo kikuu katika kambi maalum mkoani Dodoma, nao ukaweka kiashiria 'mama kaupiga mwingi.'

Ni siku chache zilizopita, Rais Dk. Samia amesema ni mradi uliowagusa vijana sasa umevutia wageni zaidi kuwekeza na kuendeleza mradi, ambao unachukua sura ya uzalishaji wa kisasa, bora unaopanua wigo wa ajira kwa kizazi kipya katika jamii.

Serikali ya Awamu ya Sita, pia inafungua wigo wa kilimo kwa uzalishaji huo wa kisasa, unaoasisiwa sana na wataaluma kama TARI na wasomi wenza wao, SUA, kwa harakati zinazoendelea kuboresha uzalishaji mbolea, ikiwekeza jicho mbali nchini kuwe soko kuu la Bara Afrika, maana yake nyumbani kutajitosheleza na kilimo kitapaa.

Hivi karibuni nchini kuimekuwapo kongamano la kilimo la Bara la Afrika nchini na moja ya sura za majumuisho ilikuwa soko kubwa la mazao ya Afrika, huku Tanzania chini ya Rais Samia, ikilenga kumudu soko hilo.

Sera ya Mambo ya Nje sasa ipo katika Diplomasia ya Uchumi. Jicho na sauti kutoka kwa wanadiplomasia wa Kitanzania sasa, ni kuzama pia katika bidhaa ya kiuchumi kuzama katika soko la kimataifa.

Hadi sasa kuanzia msimu wa bajeti uliopo serikali imezuia kuuza holela mazao ya kilimo, badala yake imeweka utaratibu maalum iwe na tija katika soko la kumnufaisha muuzaji wa awali mkulima, vilevile juhudi za kujenga maghala ya chakula kila mkoa zikiendelea. Hadi sasa maghala hayo yanahesabika katika kikao kadhaa wazalishaji wa nafaka kitaifa.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Anayetaka kubebwa kama jeneza mwacheni abebwe!'






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

WAFUGAJI huishi na wanyama wapole na wakali, kwa madhumuni mbalimbali. Wapole huwa ni kwa ajili ya chakula, lakini wakali kwa ajili ya ulinzi.

Vijijini ni nadra sana kukuta mfugaji ana ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika, akaacha kufuga mbwa kwa ajili ya kumsaidia kulinda mifugo yake.

Lakini, anajua ni wakati gani mnyama anakasirika na wakati upi ana furaha, hususani kwa mbwa, hali hiyo hujionyesha waziwazi na hivyo mbwa akichokozwa au akifanyiwa ukatili hutafuta jinsi ya kujihami.

Unaweza kukaa mahali nyumbani kwa mtu, ukabaini kabisa urafiki au uadui wa mbwa na mfugaji wake. Ukiona mbwa anamkwepa mtu, ujue ana kisa naye na hataki kumsogelea.

Kwa maana hiyo, mbwa humjua mbaya wake na hatapenda akae naye, akimwona karibu hujitenga naye na kama ana urafiki naye, utamwona akitikisa mkia na kumkaribia na hata kumlamba kama ishara ya upendo.

Kuna simulizi ya Wafaransa ambayo inathibitisha hali hii, hususani kwa mbwa aliyeparamiwa na lori siku moja, lakini akanusurika na kuuguza majeraha hatimaye akapona.

Mbwa huyu alijenga chuki kwa malori yote yaliyokuwa yakipita mtaani kwao na kila alipoona moja alilikimbilia huku akibweka akikusudia kulipiza kisasi cha kugongwa.

Watu walioshuhudia hali hiyo, ndipo wakaibuka na usemi: 'Le chien abois la caravane passe,' kwamba 'hata mbwa abweke, lori litapita tu'. Maana ya usemi huo ni kwamba, mbwa yule hawezi kutikisa lori. Kwamba ataishia kubweka na lori litajipitia na kuendelea na safari yake.

Siasa zetu leo Tanzania zinanikumbusha usemi huo wa Wafaransa, kwamba kunaweza kuwa na watu walishaathiriwa na mfumo huko nyuma na hivyo kisaikolojia kutibuka na kujikuta hawajali kinachoendelea.

Watu hao kwa uchungu walionao, wanaona hapana haja ya kuogopa kuvamia lori, kwa sababu lilishawagonga na kusalimika, baada ya kukaribia kuonja umauti.

Hivi karibuni, serikali imekuwa ikikwazika sana na kinachoendelea kutoka kwa wanasiasa wa upinzani, ambao wamekuwa wakizunguka karibu kila kona ya nchi kuhanikiza wanachoamini kitawafaa wananchi.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimo katika hilo. Hivi karibuni, Makamu Mwenyekiti wake na mwanasheria msomi, Tundu Lissu, alijikuta matatani pale alipotaka kuingia Ngorongoro.

Lissu na ujumbe wake, kama ambavyo walikuwa wamefanya katika maeneo mengine, wakihubiri kwa kina mikataba ya kiserikali wasiokubaliana nayo, pia wakidai Katiba Mpya, ije, walitaka wakayaeneze huko Ngorongoro.

Walizuiwa kwa nguvu ya dola na wakashindwa kuingia Ngorongoro na kusababisha taharuki kwa wafuasi wa chama hicho, pia kwa baadhi ya wakazi wa eneo hilo, waliodai kumsubiri kwa hamu.

Ukafika wakati hata Chifu Hangaya, kwa nafasi yake naye akashindwa kuvumilia na kujikuta akihanikiza kukerwa na tabia ya wanasiasa hao kutoa maneno makali, badala ya kutumia alichokiita fursa ya ruhusa ya uhuru wa mikutano, kujiimarisha kwa kuhubiri mema na kupata wanachama.

Mama akasema kinachoonekana na kwamba baadhi ya wanasiasa wameishiwa cha kusema, na ndiyo sababu wanarukaruka, leo Katiba, kesho Bandari na kurudi tena kwenye Katiba, badala ya kujipanga kwa uchaguzi ujao.

Upande wa Lissu na wenzake, nao tukawasikia ukaja juu na kuhoji kisa cha kuzuiwa kuingia Ngorongoro, kana kwamba huko kuna wafungwa wasiotakiwa kuonwa na wanasiasa, huku wakazi wa Ngorongoro, nao wakihanikiza kwa lugha hiyo hiyo, kwamba wao si wafungwa wa kutengwa.

Ieleweke tu, kuwa Lissu amepitia kipindi kigumu sana maishani mwake, kumiminiwa risasi zote zile mpaka kuachwa na ulemavu wa maisha si kitu kidogo. Kisaikolojia lazima ametibuka na hivyo huenda haogopi lolote.

Hivyo alitakiwa kuchukuliwa kinamna fulani hivi na kumwacha aendelee na alichokusudia kukifanya, ili mradi hakuwa anavunja sheria ya mikutano ya hadhara.

Ningekuwa mimi ni Mamlaka, Lissu ningempa ulinzi mzito na kumsindikiza na askari wengi hata kama na vifaru na kumepeleka Ngorongoro na kumsimamia akafanya mkutano wake bila bughudha.

Wananchi wa Ngorongoro wenyewe wangeamua, kama alichowapelekea ni pumba au mchele na kubaki na uamuzi wao, vinginevyo tungechukua kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ya miaka ya tisini.

Alipoona Augustine Mrema anasumbua, akibebwa na wananchi, alisimama pale Jangwani, akasema anayetaka kubebwa kama jeneza mwacheni abebwe. Mbona yaliisha na mambo yakaendelea kama kawaida?

**Alamsiki!**

BIASHARA

# Waziri mpya Biashara atinga kiwandani kuthibitisha anakaribisha PPP, uwekezaji

## • Ahakikishiwa mambo safi, mrejesho zawadi kapewa mkulima

**Na Frank Monyo**

DIRA ya serikali sasa, ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara. Tayari jitihada za kutekeleza hilo zinafanyika na sasa, mradi wa kituo kikubwa cha biashara (shopping mall) kinachojengwa Ubungo mkoani Dar es Salaam, ujenzi wa viwanda, wawekezaji kuonyesha nia ya kuwekeza nchini ni kielelezo cha safari hiyo.

Rais Samia Suluhu Hassan, katika moja ya hotuba zake hivi karibuni, akanukuliwa akisema, “Sekta binafsi ni mhimili muhimu wa maendeleo ya nchi kwa sababu huchangia kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi, huku akisisitiza hakuna taifa lolote duniani ambalo linaweza kupiga hatua ya maendeleo bila kushirikiana na sekta binafsi.

Akatoa agizo kwa mawaziri wa sekta mbalimbali kukaa na kujadiliana na wafanyabiashara wa sekta binafsi kuendelea kutatua changamoto zinazowakabili, ikiwamo kuweka mazingira rafiki ya biashara ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

Hata Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, naye amewakaribisha wawekezaji kutoka Umoja wa Ulaya (EU), kuwekeza nchini katika sekta za Kilimo, Usafirishaji, Nishati,Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Utalii na katika viwanda, kuongeza thamani ya bidhaa, kwa kuwa serikali inahitaji kufungua zaidi sekta hizo kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Makamu wa Rais alitoa kauli hiyo mapema mwaka huu wakati akifungua Jukwaa la Kwanza la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Umoja wa Ulaya linalofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

Akasema, Tanzania imedhamiria kuvutia uwekezaji katika kutumia rasilimali zilizopo kwa kuzingatia eneo la kimkakati, iliyopo, ambayo ni fursa ya kuhakikisha usalama wa chakula pamoja na ukuzaji wa kilimo kwa ujumla unakuwapo.

Rai ya kiongozi huyo kitaifa, ambaye pia ni mchumi kitaaluma, sasa Tanzania ipo katika maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa kwa miaka mingine 25, inayolenga kubadilisha uchumi wa nchi, kutoka katika ngazi ya kati chini hadi kufikia uchumi wa kati juu, ambao kwa kiasi kikubwa unahitaji wa biashara na uwekezaji.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Serengeti (SBL), Obinna Anyalebechi, baada ya kufanya ziara katika ofisi za kampuni hiyo, ikiwa sehemu ya kuendeleza urafiki wa sekta binafsi na umma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**WAZIRI WA BIASHARA**

Waziri mpya wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, katika hilo ameonyesha msisitizo wake, katika ziara aliyofanya kwenye Kampuni ya Serengeti (SBL) na kuueleza uongozi wa kampuni hiyo, kuwa serikali inaendelea kusisitiza dhamira yake kupitia upya sera na mfumo wa kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Dk. Kijaji katika mazungumzo yake na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, anasema hiyo ni katika jitihada za kufanya Tanzania kuwa eneo kuu la uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Hapo akamhakikishia, kuwa serikali iko tayari kufanya mazungumzo na sekta binafsi kama njia ya kutatua changamoto zinazokabili wafanyabiashara nchini katika nafasi zao.

> **“Upanuzi huu umesababisha kuongezeka kwa uzalishaji na kwa hiyo kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa serikali kutoka kwa biashara yetu, wakati unaimarisha uwezo wa kampuni kufadhili programu za kusaidia jamii zaidi,” anasema Mkurugenzi Mtendaji.**

“Sekta binafsi ni mdau muhimu katika ujenzi wa taifa. Tunathamini jukumu la sekta hii katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi, mchango wake katika kutengeneza ajira, ukusanyaji wa mapato ya serikali, na misaada kwa jamii,” anasema Dk. Kijaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Obinna Anyalebechi, akamshukuru Waziri Dk. Kijaji, kwa msaada wa wizara kwa sekta binafsi, jambo analoeleza linaongeza shauku na ujasiri wa wawekezaji nchini Tanzania.

Anasema, SBL imewekeza zaidi ya Sh.bilioni 165 katika miaka mitatu iliyopita kwa lengo la kuongeza uzalishaji bia na vileo kwa kupanua uwezo wa viwanda vyake, jambo lililotatua ajira mpya na kuongeza fursa kwa wazalishaji wa ndani kwa kampuni hiyo.

“Upanuzi huu umesababisha kuongezeka kwa uzalishaji na kwa hiyo kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa serikali kutoka kwa biashara yetu, wakati unaimarisha uwezo wa kampuni kufadhili programu za kusaidia jamii zaidi,” anasema Mkurugenzi Mtendaji.

Programu za Kusaidia Jamii za SBL, kulingana na Obinna, zinajumuisha uchimbaji visima vya maji na usambazaji huduma ya maji, upandaji miti, na mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana, wanawake, na makundi yanayotengwa.

Mikoa ambayo mradi wa uchimbaji wa visima vya maji umetekelezwa ni; Iringa, Singida Kilimanjaro, Mwanza, Tanga, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani, Dodoma na Mara ambako watu zaidi ya milioni mbili wamefaidika na upatikanaji wa maji katika maeneo hayo.

Kampuni hiyo pia inaendesha programu ya kilimo inayosaidia zaidi ya wakulima wa ndani 400 wanaolima mazao ya shayiri, mahindi, mtama, na nafaka nyingine ambazo kampuni inanunua na kutumia kama malighafi kwa uzalishaji wa bia.

Pia kampuni ya SBL inatoa ufadhili wa masomo ya kilimo kwa vijana wa Kitanzania wanaotoka kwenye familia zenye kipato duni.Ufadhili huo unaotolewa kila mwaka, unatolewa chini ya programu ya SBL inayojulikana kama ‘Kilimo Viwanda’ ambao wanafuika hulipiwa gharama zote za masomo na kwa kipindi chote wanachokuwa wakijifunza.

Programu ya ‘Kilimo Viwanda’ ilianzishwa na SBL mwaka 2019, ikilenga kusaidia kuongeza wataalamu wa kilimo kupitia kutoa ufadhili wa masomo.

Wanafuika wa programu hiyo ni vijana wa Kitanzania wenye ufaulu mzuri darasani, ambao wanatokea katika familia zenye kipato duni.

Katika utekelezaji wa programu, SBL imeingia ubia na vyuo vinne vya ndani vinavyofundisha fani ya kilimo, ambavyo hupokea wanafunzi wanaolipiwa kupitia programu hii.

Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo cha Kilimo na Mifugo Kaole Wazazi kilichopo Bagamoyo, mkoani Pwani, Chuo cha Kilimo na Mifugo cha Kilacha kilichopo Moshi, Kilimanjaro, Chuo cha Kilimo Mt. Maria Goretti kilichopo Iringa na chuo cha Kilimo Igabiro, kilichopo Muleba mkoani Kagera.





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo (kulia), akiwa katika kikao na Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa (wa pili kushoto), Ofisini kwake katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma jana.. Kushoto ni Mshauri wa Uchumi wa Ubalozi huo, Christopher Ntyangiri. **PICHA: OMR**

# JKT waomba ndege zisizo na rubani kufanya doria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) kikosi cha Makutupora jijini hapa, kimeomba serikali kuipatia ndege zisizo na rubani (drone) kusaidia doria katika Bonde la Mzakwe ambalo ni chanzo kikuu cha maji Jiji la Dodoma ili kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Kaimu Kamanda wa Kikosi cha 834 JKT Makutupora, Meja James Macheta kwenye sherehe za kuhitimu mafunzo kwa vijana kwa mujibu wa sheria, Operesheni ya miaka 60 ya JKT.

Alisema bonde hilo limekuwa likikumbwa na uharibifu wa mazingira ikiwamo kuchoma moto na kusababisha miti wanayoitunza kukauka.

"Hawa wahitimu wameshiriki kutunza mazingira hasa miti iliyopandwa kwenye bonde hili, hivyo drones zitakapopatikana zitasaidia kufanya doria kwa muda mfupi kwa ufanisi na kuweza kufika eneo lote la bonde,"alisema.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliahidi kulichukua ombi hilo na kuwasiliana na Wizara ya Maji ili kuhakikisha vifaa hivyo vya kulinda bonde hilo vinapatikana.

Hivi karibuni, uongozi wa Bonde la Wami/Ruvu ambao Bonde la Mzakwe lipo chini yake, ulitaja mikakati ya kuweka vikinga moto ili kulinda miundombinu ya uzalishaji maji katika eneo hilo.

Mkurugenzi wa Bonde la Wami/Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmassy, alisema kutokana na matuko ya mara kwa mara ya moto katika hifadhi hiyo wameamua kuweka vikinga moto ili kulinda miundombinu na vyanzo vya maji katika eneo hilo linalotegemewa kwa zaidi ya asilimia 90 kuhudumia wakazi wa Dodoma.

Mmassy, alisema pamoja na kuweka vikinga moto lakini pia watashirikiana na JKT kuendesha doria kwenye eneo hilo ili kuzuia matukio ya watu kuchoma moto katika eneo hilo.

"Hifadhi hii ya vyanzo vya maji ipo chini ya Bonde la Wami/Ruvu na chanzo hichi ni chanzo muhimu sana ambacho kinategemewa kwa asilimia 90 ya uzalishaji wa maji katika Jiji la Dodoma" alisema

Aidha, alisema lengo la kuweka vikinga moto katika eneo hilo ni kupunguza athari ambazo zimekuwa zikijitokeza katika hifadhi hiyo ya vyanzo vya maji.

# Vyama vya msingi Singida vyadaiwa mil.300/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

VYAMA vya msingi mkoani Singida vinadaiwa Sh. milioni 300 baada ya kushindwa kununua pamba kutoka kwa wakulima katika msimu wa kilimo mwaka 2022/23.

Fedha hizo zilitolewa na kiwanda cha kuchambua pamba kiitwacho Biosustain (T) Limited mkoani hapa kwa vyama vya msingi zaidi ya 40 ili wanunue pamba kutoka kwa wakulima.

Meneja wa kiwanda hicho, Salum Halfan Salum, alitoa taarifa hiyo jana wakati kizungumza na waandishi wa habari.

Alisema fedha hizo zilipelekwa katika vyama vya msingi katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 kwa ajili ya kununua pambana lakini zilibaki Sh.milioni 300 ambazo zilitakuwa kurejeshwa.

Alisema fedha hizo wanazidai kwa vyama vya msingi vipatavyo 40 kutoka wilaya za Meatu na Maswa mkoani Shinyanga na vilivyopo katika Mkoa wa Singida.

Salum alisema kiwanda hicho kimekuwa kikinunua pamba kwa karibu asilimia 96 kutoka kwenye vyama vya msingi, utaratibu ambao umekuwa ukitumika ni kupeleka fedha kwenye vyama hivyo ambavyo navyo hununua pamba kwa wakulima.

Alisema katika hali ya kushangaza baadhi ya viongozi wa vyama vya msingi waliofanya ubadhirifu wa fedha hizo wameachishwa kazi bila kuchukuliwa hatua.

Kufuatia hali hiyo, ameiomba ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini kuingilia kati ili fedha hizo ziweze kurejeshwa kwani baadhi ya viongozi waliohusika wameondoshwa kwenye uongozi.

Salum alisema changamoto nyingine wanayopata katika ununuzi wa pamba ni baadhi ya wakulima kuchanganya mchanga kwenye pamba ili kuongeza uzito jambo ambalo limekuwa likiondoa ubora wa zao hilo.

# Serikali yakumbushwa kutimiza SDGs, kuwajali walemavu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ILI kufanikisha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ifikapo mwaka 2030, serikali imetakiwa kuweka kipaumbele cha kwanza katika masuala ya mipango, programu na bajeti ili kuwahudumia watu wenye ulemavu.

Wadau wa kutetea na kuwasaidia watu wenye ulemavu nchini walibainisha hayo jana jijini hapa, walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa malengo hayo 17 ambayo utekelezaji wake umepangwa kukamilika ifikapo mwaka 2030.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Walemavu la Masuala ya Kisheria na Maendeleo ya Uchumi wa Jamii (DOLASED) nchini, Wakili Gidion Mendesi, alisema ili Tanzania kufanikiwa katika utekelezaji wa malengo hayo inapaswa kuweka programu jumuishi kwa watu wenye ulemavu.

"Ili kufanikiwa utekelezaji wa malengo haya 17 ya maendeleo endelevu serikali hainabudi kuhakikisha kuwa mipango yote ya maendeleo inajumuisha watu wenye ulemavu," alisema.

Aidha, alisema katika mipango yote inayotekelezwa na serikali makundi yaliyoachwa nyuma yanapaswa kupewa kipaumbele kwa kujumuisha kwenye mipango yote ya maendeleo.

"Kama malengo haya yanavyosema hakuna kumuacha mtu yoyote nyuma, hivyo ipo haja kwa serikali kuhakikisha kuwa malengo haya yanatekelezeka lakini kwa kujumuisha makundi yote yaliyoachwa nyuma hasa wanawake na wasichana wenye ulemavu ambao wengi wao bado wanakabiliwa na umaskini, njaa na mabadiliko tabia nchi" alisisitiza Mendesi

Kadhalika, alimuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasilisha mbele ya wakuu wa nchi na serikali katika mkutano wa wakuu wa malengo ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UN) mjini New York, Marekani ombi la kuwa na mpango kazi.

Alisema mpango kazi huo utasaidia kuongeza ushiriki na ujumuishwaji wa wanawake na wasichana wenye ulemavu katika michakato ya utekelezaji na ufuatiliaji wa SDGs katika ngazi ya nchi na kimataifa.

"SDGs ni mkusanyiko wa malengo 17 kabambe ambayo yanalenga kupunguza umaskini na ukosefu wa usawa ifikapo mwaka 2030 ambayo yalipitishwa mwaka 2015 na UN na serikali duniani kote" alisema

Alisema katika muda usiozidi mwezi mmoja katika hatua ya katikati ya utekelezaji wa SDGs nchi wanachama zitakusanyika katika mkutano wa SDG mjini New York Marekani kufanya ahadi mpya ra kutathimini maendeleo.

Mendesi, alisema ili kuleta mabadiliko endelevu kufikia SDGs na kujenga dunia yenye usawa zaidi watoa maamuzi wa kimataifa hawawezi kuendelea kupuuza asilimia 16 ya watu duniani ambao wanaulemavu.

Ofisa wa Sheria wa Chama cha Albino Tanzania (TAS), Saleh Alex, alisema kama ripoti ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa inavyoonyesha watu wenye ulemavu wanaathirika zaidi na ukosefu wa maendeleo, umaskini na ukosefu wa usawa.

"Ulimwenguni watu wenye ulemavu wanaishi chini ya mstari wa umaskini kuliko wasio na ulemavu ikiwa ni pamoja na waiishio Tanzania," alisema

Hata hivyo alisema wanatoa wito kwa viongozi wa Tanzania kuhakikisha utekelezaji wa SDGs na kuhakikisha kuwa wanajumuisha watu wenye ulemavu katika utekelezaji wake.

Alisema: "Viongozi wa Tanzania wanapaswa kuhakikisha kuwa azimio la kisiasa na ahadi zote za kitaifa zilizotolewa zinalenga kuwafikia wale wanaoachwa nyuma zaidi hii ni nafasi yetu ya mwisho kurudisha malengo kwenye mstari".






Mkuu wa wilaya ya Temeke, Mobhare Matinyi (wapili kushoto), akipokea vifaa vya usafi kutoka kwa Mwakilishi wa kikundi cha Tirima wakati wa zoezi la uzinduzi wa wiki ya usafi katika kata ya Kurasini, Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Elihuruma Mabelya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Moto wateketeza madarasa Shule ya Sekondari Iyela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MATUKIO ya shule kuungua yamerejea tena mkoani hapa, baada ya moto ambao chanzo chake hakijafahamika kuteketeza vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Iyela mkoani hapa, huku vingine vikinusurika baada ya wananchi kuudhibiti moto huo.

Moto huo ulizuka juzi asubuhi wakati wanafunzi wa kidato cha nne wakiendelea kujisomea shuleni hapo katika kipindi hiki ambacho shule zimefungwa.

Wakizungumza na wandishi baada ya moto huo kudhibitiwa, walimu wa shule hiyo walisema chanzo cha moto huo bado hakijulikani licha ya kuwepo uvumi kuwa kuna mwanafunzi alionekana akikimbia, huku akiwa ameshikilia moto.

Mwalimu Devotha Hoza alisema akiwa nyumbani kwake alipata taarifa kutoka kwa mwalimu mwenzake kuwa kuna moto unawaka shuleni na ndipo akakimbia kwenda kuokoa vitu vilivyokuwemo ndani ya vyumba hivyo.

Alisema alipofika alikuta moto ni mkubwa halafu baadhi ya wanafunzi wakawa wanataka kuingia kwenda kuokoa vitu vyao yaliwemo magodoro na ndipo akawazuia na kuwashauri waendelee kuuzima moto huo kwa kutumia vumbi.

Alisema moto huo haukuwadhuru wanafunzi zaidi ya kuteketeza vitu vyao vilivyokuwemo zikiwemo daftari, magodoro na vitu vingine ambavyo walikuwa wamehifadhi kwenye vyumba hivyo.

"Kuna mtoto wa shule ya msingi amesema alimuona mwanafunzi wa sekondari akiwa ameshika moto anakimbia nao kuja huku, tuna wasiwasi kwamba moto huu utakuwa umewashwa kwa makusudi kabisa," alisema Mwalimu Devotha.

Naye Mwalimu Charles Hoza ambaye ni balozi wa eneo ilipo shule hiyo, alisema alipopata taarifa ya moto huo alianza kupuliza filimbi na 'vuvu zela' kwa lengo la kuwataarifu wananchi kuwa kuna tukio la hatari katika eneo hilo.

Alisema mbali na kupuliza vifaa hivyo pia alitangaza kuwa kuna ajali ya moto shuleni na hivyo wananchi wanaakiwa kwenda kusaidia kukabiliana nao.

Alisema wananchi walijitokeza kwa wingi na wakafanikiwa kuudhibiti moto huo kabla haujaanza kuunguza madarasa mengine na kwamba gari la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilikuwa linafika katika eneo hilo wakati wananchi wamefanikiwa kuudhibiti moto.

"Nilipata taarifa saa 1:27 asubuhi kupitia kwa mwalimu Joyce, nawashukuru sana wananchi wa eneo hili ambao walijitokeza kwa wingi sana kukabiliana na moto huu, wamefanya kazi kubwa na ndiomaana maeneo mengine yamepona," alisema Hoza.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Iyela Moja, Salim Njechele alisema baada ya kupata taarifa za ajali hiyo aliwatafuta viongozi wa kata hiyo kwa ajili ya kusaidia kuhamasisha wananchi kujitokeza kuuzima.

Alisema mbali na viongozi wa kata hiyo pia alipiga simu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya kuwaomba msaada na kwamba muda mfupi baadaye walifika na kushirikiana na wananchi kuzima maeneo ambayo moto ulikuwa umebakia.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mkoa wa Mbeya, Mrakibu Malumbo Kata alisema walipopata taarifa waliwahi eneo la tukio na kukuta wananchi wanaendelea kupambana kuzima moto huo.

Alisema walishirikiana kuuzima lakini ukiwa tayari umeteketeza vyumba viwili vya madarasa pamoja na vitu vyote vilivyokuwemo ambavyo wanafunzi wanavitumia.

Alisema chanzo cha moto huo bado hakijabainika lakini wanaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo hicho na kuchukua hatua zaidi.

# Watoto wanaoishi mazingira magumu wakatiwa bima ya afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO 10 wanaoishi kwenye mazingira magumu katika Wilaya ya Mbeya wamenufaika na msaada wa kukatiwa bima za afya ili kuwasaidia kupata matibabu.

Msaada huo ulitolewa na kikundi cha wanawake kiitwacho Exodus Women Group kinachoongozwa na Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Elizabeth Lyombe.

Alisema kikundi hicho kiliamua kuanza kutoa misaada hiyo kutokana na kubaini kwamba watoto wengi wanaoishi kwenye mazingira magumu wanapata matatizo ya kiafya lakini wanashindwa kutibiwa na baadhi wanakosa mahitaji muhimu.

Alisema kikundi hicho kinawasaidia zaidi watoto ambao wanalelewa kwenye familia maskini tofauti na vikundi vingine ambavyo huwa vinawasaidia watoto wanaoishi kwenye vituo vya kulelea watoto yatima.

"Tulianza Mwaka jana kwa kuanza na watoto watano ambao tuliwakatia bima za afya na leo tunawakabidhi watoto 10 bima pamoja na mahitaji muhimu lakini tutaendelea kufanya, hivyo ili kulisaidia kundi hili muhimu kwa taifa," alisema Lyombe

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Emiliana Mbise, alikishukuru kikundi hicho kwa msaada huo akidai kuwa wapo watoto wengi ambao wanaishi kwenye mazingira magumu.

Alivitaka vikundi vingine pamoja na watu wenye uwezo wa kiuchumi kuyasaidia makundi maalumu kwa maelezo kuwa misaada hiyo inasaidia kuzifariji familia hizo.

# DC aagiza kubandikwa bei za mbolea kanisani, msikitini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kassongwa amewaagiza mawakala wilayani humo kufuata bei elekezi ya uuzaji wa mbolea sambamba na kubandikwa kwa bei hizo kuanzia ngazi ya kitongoji, vijiji, kanisani na msikitini ili zijulikane kwa wananchi

Kassongwa aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye kikao cha wadau wa mbolea ambapo pia aliagiza halmashauri zote za Wilaya ya Njombe kuongeza muda wa usajili kwa wakulima.

"Hao ambao watakuwa hawajasajiliwa watakuwa kwenye taharuki kwa sababu hiyo ni kero kwa wakulima naona vitu vingine havipaswi kuwa kero naomba hili lifanyike mara moja kuanzia kesho, madaftari yarudi site watu waendelee kujisajili na itafutwe namna nzuri ya kuchukua data na kuja kuzisajili kwenye softcopy (nakala laini)"alisema Kasongwa.

Alisema ni vema kipindi hiki mawakala waondoe makandokando yaliyotokea kipindi kilichopita.

"Tuepuke kufanya udanganyifu, tushirikiane tutoe haki kwa watu wasiuziwe bei ambayo siyo na hizi bei elekezi ninaelekeza wananchi zibandikwe kwenye mbao za matangazo vijiji vyote kwa sababu hakuna sehemu isiyotajwa naomba Katibu Tawala bei hizi zishuke hadi kwa watendaji wa vijiji wabandike kwenye ofisi zote, kwenye sehemu zote za jumuiya, makanisani misikitini ili mtu asije akaja akasema alikua hafahamu,"alisema Kasongwa.

Meneja wa Kanda wa Nyanda za Juu Kusini wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), Michael Sanga, alitoa wito kwa wananchi wa Wilaya ya Njombe kwamba wahimizwe kujiandikisha kwenye kitambulisho cha taifa ili waweze kupata namba za nida.

"Huko tunakoelekea tutaamua kwamba sasa ndio uwe utaratibu maalumu vinginevyo mkulima hataweza kujiandikisha kwenye mfumo tena, pia tutumie majukwaa yetu kuwahimiza wakulima jamani mkajiandikishe kwa sababu hakuna gharama yoyote," alisema Sanga.

Mwenyekiti wa Mawakala wa Mbolea Mkoa wa Njombe, Asifiwe Magoma, alisema kazi nzuri iliyofanya na serikali inawafanya mawakala kuonekana siyo wezi tena.

Alisema: "Waziri Bashe ametutengenezea mfumo mzuri ambao unaonyesha wazi kwamba ukitekeleza zoezi hili nje na utaratibu unaonekana mara moja lakini pia niwaombe mawakala tukafanye kazi kwa uaminifu ili tuweze kuaminiwa na serikali".



# Waganga tiba asili waliosajiliwa Zanzibar wafikia 600

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema idadi ya waganga wa tiba asili visiwani hapa waliosajiliwa hadi mwaka jana ni 600.

Wamesema mtu yoyote anayehitaji kusajiliwa anatakiwa kuwasilisha kwa mrajis nyaraka muhimu za utambulisho wake.

Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Amei Abdallah Ameir aliyetaka kujua taratibu na vigezo ambavyo vinatumika kuwasajili waganga wa tiba asili.

Mazrui alisema miongoni mwa vigezo vinavyohitajika mtu kusajiliwa ni awe na shahada au cheti kinachohusiana na tiba mbadala kutoka taasisi inayotambulika.

Alisema kwa bahati mbaya Zanzibar haina chuo ambacho kinatoa elimu ya tiba asili na tiba mbadala na badala yake waganga hao hupatiwa mafunzo ya muda ili kuhakikisha tiba wanazozitoa hazileti athari kwa jamii.

"Mganga wa tiba asili na tiba mbadala anatakiwa kuwa na hati yoyote muhimu ya kuthibitisha ujuzi huo," alisema Mazrui. Alisema mganga pia anaweza kupewa usajili wa awali au usajili kamili kulingana na sifa na vigezo alivyonavyo. Alisema waganga wa tiba asili na mbadala watalipia tozo ya Sh. 80,000 ya usajili wa awali na kwa kila mwaka watatakiwa kuhuisha kibali chao kwa Sh.25,000.

Akijibu swali lingine la mwakilishi huyo aliyetaka kujua ni tafiti gani ambazo zimefanywa kutoka katika maabara za afya jamii na kuleta matokeo chanya, Mazrui alisema maabara za jamii zilifanya utafiti mbalimbali zikiwemo za maradhi ya kichocho, minyoo, afya ya mama na mtoto na ugonjwa wa virusi vya corona.

Alisema utafiti wa kichocho ulifanyika katika majimbo 45 ya Pemba na matokeo yalionesha kupungua kwa ukubwa wa tatizo hilo kutoka asilimia nane hadi asilimia tatu.

Aidha, alisema utafiti wa mama na mtoto unaendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Wete na Chakechake Pemba kwa mama wajawazito wa wiki nane hadi 19 kwa lengo la kuangalia sababu zinazosababisha matatizo ya uzazi kwa kinamama.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari Kitope, Mkoa wa Kaskazini Unguja, wakiwa katika foleni ya kuingia chooni jana, kutokana na uhaba wa vyoo shuleni hapo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Shule yakabiliwa uhaba wa vyoo, madawati, madarasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHULE ya Msingi na Sekondari Kitope iliyopo mkoani Kaskazini Unguja inakabiliwa na tatizo la uhaba wa vyoo, madarasa, madawati kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi.

Hali hiyo inasababisha darasa moja kuwa na idadi ya wanafunzi 90 kwa elimu ya msingi.

Wakizungumza mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahoud katika muendelezo wa mikutano yake na wananchi kusikiliza kero zinazowakabili, wanafunzi hao walisema uhaba wa vyoo umewasababisha kutumia choo pamoja wanafunzi wa kike na kiume.

"Vyoo viliopo ni vichache hasa wakati huu ambapo sisi wanafunzi wa darasa la saba, kidato cha pili na nne tunakabiliwa na mitihani ya taifa, tupo hapa kwa muda wote asubuhi hadi usiku kwa ajili ya kujisomea" alisema Mwanafunzi Rabia Abdallah wa shule hiyo.

Aidha, aliiomba serikali kuwajengea vyoo vyengine pamoja na kuongeza ujenzi wa madarasa ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira mazuri na kufanya vizuri katika mitihani yao.

Mwalimu wa Sekondari wa Shule hiyo, Ali Afadhali, alisema shule hiyo kwa sasa ina vyoo sita vinavyotumika, vyoo 12 ni vibovu havitumiki, kwamba idadi ya wanafunzi ni 1,700 kwa sekondari na 530 msingi.

"Vyoo 12 ambavyo havitumiki miundombinu yake ni mibovu na havifai kabisa kutumika, hivyo tunaupungufu wa vyoo na wanafunzi kulazimika kukaa foleni kusubiriana wanapohitaji mahitaji ya choo" alisema.

Ofisa Elimu Mkoa wa Kaskazini Unguja, Muhammed Mzee Choum, alisema shule hiyo imezidiwa na idadi kubwa ya wanafunzi hali ambayo inasababisha darasa moja kuwa na wanafunzi 86 idadi ambayo ni mara mbili kwa mahitaji.

Alisema kwa mujibu wa sera ya elimu darasa moja hutakiwa kuwa na wastani wa wanafunzi 45 na Wizara ya Elimu inatarajia kujenga shule ya ghorofa katika shule hiyo ili kuondokana na tatizo hilo.

Kuhusu uhaba wa walimu, alikiri uwapo wa tatizo hilo ambalo halipo kwa Shule ya Kitope pekee bali kwa shule nyingi za msingi katika mkoa huo, kwamba kuna uhitaji wa walimu 456 wa shule za msingi ili kuondoa tatizo hilo.

Alisema serikali inatarajia kutekeleza mradi wa kuajiri walimu 1,002 ambapo Mkoa wa Kaskazini utapata mgawo wa walimu 80.

Aidha alisema kwa sasa serikali imejikita katika ujenzi wa madarasa na Zanzibar inauhitaji wa madarasa 5,000, hivyo bado kuna uhaba.

Kuhusu uhaba wa madawati alikiri uwepo wa changamoto hiyo akisema kwa sasa serikali inatekeleza mradi wa kuweka madawati katika shule zote za sekondari.

# Mfumuko wa bei Zanzibar waongezeka, wafikia 6%

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIWANGO cha mfumuko wa bei kwa Agosti mwaka huu kimeongezeka hadi asilimia 6.82 kutoka asilimia 6.70 ilivyosajiliwa Julai 2023.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Bei, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salma Saleh Ali, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kiwango cha mfumuko huo kilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji visivyo na vileo kwa asilimia 11.66 kwa kipindi cha Agosti 2023 ikilinganishwa na asilimia 11.51 kipindi cha Julai.

Aidha, alisema, faharisi za bei ziliongezeka hadi 107.15 kipindi mwezi Agosti ikilinganishwa na 100.31 mwezi Agosti 2022. Alizitaja bidhaa zilizosababisha ongezeko hilo ni pamoja na mchele wa mapembe asilimia (32.72), mchele kutoka Mbeya (20.90), unga wa ngano (12.66), unga wa sembe (28.18), ndizi za mkono mmoja (8.68), ndizi za mtwike (3.66) na sukari nyekundu (36.08).

Mchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk.Ulrick Mumburi, alisema, kupanda na kushuka kwa mfumko wa bei ni hali ya kawaida kulingana na mwenendo wa kibiashara. "Lakini mfumuko unapopanda au kushuka kwa kasi kubwa, athari yake ipo moja kwa moja na yenye kutishia kiuchumi" alisema mchumi huyo. Aliongeza: "Bidhaa zitakapokuwa bei ya juu itakuwa mzigo kwa mtumiaji, lakini, zikishuka sana mzalishaji atashindwa kuendelea na uzalishaji".

Hata hivyo, alisema, bado hali ya kiuchumi inabakia vizuri kutokana na kuwepo kwenye tarakimu moja ambayo ndiyo njia bora ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**(CAP 117)**
**DEED POLL**

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made this 04th day of August 2023 by me **ISAYA ABRAHAM MWANTEPELE** of P.O.Box 337,Mbeya,an adult Christian, DO HEREBY state that the name **ISAYA A.MWANTEPELE** appeared in my Vote Card while the name **ISAYA ABRAHAMU MWANTEPELE** appeared in my marriage certificate while the name ISAYA ABRAHAM MZUMBWE appeared in my national identification.

That,by this deed I absolutely renounce and abandon the use of the name **ISAYA ABRAHAM MZUMBWE** and the name **ISAYA A.MWANTEPELE** and substitute by the name **ISAYA ABRAHAM MWANTEPELE.**

**AND IN PURSUANCE** of such change of name as aforesaid **I DECLARED** that I shall at all times hereafter in all records,documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the name of **ISAYA ABRAHAM MWANTEPELE.**

**IN WITNESS** whereof I have hereunto subscribed my name of **ISAYA ABRAHAM** MWANTEPELE and have affixed my signature the year herein written.

**SIGNED AND DELIVERED by the said ISAYA ABRAHAM MWANTEPELE.**
**Letter known to me personally in my presence this 4th day of August,2023 ........................**




**BEFORE ME:**
**Name:GOOD OTTO MGIMBA**
**Signature:........................**
**Address: 2757,MBEYA**
**Qualification:COMMISIONER FOR OATH**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACTS**
**(CAP.117 RE 2019)**
**DEED POLL (CHANGE OF NAME)**

By this **DEED I,BARAKA NDOSTE MBOYA** that formerly known as **BARAKA NDOSTE SONGWE** do hereby absolutely renounce and abandon the use of the names BARAKA NDOSTE SONGWE that has been used in my Civilian identity (NIDA **No.19990724-53109-00001-26)** respectively,made prior to this changes and in lieu thereof do hereby assume and adopt the name of **BARAKA NDOSTE MBOYA** that appears in my academic certificates.

And pursuance of such change of names as aforesaid **I HEREBY** declare that I shall at all times hereinafter in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign by the name of **BARAKA NDOSTE MBOYA** as my names in lieu of this change.

The reason for such change of names is due to formalizes the names that appears in my academic certificates and,whereas I adopt the names **BARAKA NDOSTE MBOYA.**

AND,I HEREBY AUTHORIZE and request all persons and authorities to designate and address me,the names of **BARAKA NDOSTE MBOYA** only in substitution of my former names **BARAKA NDOSTE SONGWE.**

I,the said **BARAKA NDOSTE MBOYA,** make this declaration conscientiously believing the same to be true in accordance with the provisions of the OATHS (Judicial Proceedings and Statutory Declaration) Act,1966.

**SIGNED and DELIVERED by the said of BARAKA NDOSTE MBOYA is known to me ,the latter being known to me personally this 19 day of July,2023.**



**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED, I KHALDA AKBARY MKULO OF P.O. BOX, DAR ES SALAAM, DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former names of **KHALDA M. MKULO** and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of **KHALDA AKBARY MKULO.** The reason for the change of name is that there were some faults occurred on my other transactions including my CRDB bank account number **0112018532500** where my names read **KHALDA M. MKULO** instead of **KHALDA AKBARY MKULO** as it shows on my citizen identity card number **19610520-14112-00001-11.** For the purpose of evidences such determination, I hereby **DECLARE** that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **KHALDA AKBARY MKULO** as my name lieu of and in substitution for my former names of **KHALDA M. MKULO.**

**AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **KHALDA AKBARY MKULO.**

**IN WITNESS WHEREOF I** have set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old names of **KHALDA M. MKULO** by my new name of **KHALDA AKBARY MKULO.**

SIGNED and DELIVERED by the said
KHALDA AKBARY MKULO
who is known to me personally/identified
to me by ........................
the latter being known to me personally
in my presence this 23 day of May
2023
DEPONENT



Name: Qassim Abdallah
Signature: ........................
Postal address: 
Qualification:

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUSSA NDALIJANYE RAJABU** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 151 BWH – MITSUBISHI FUSO** yenye CHASSIS No. **FK417F520063.** ENGINE No. **963228.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
RB NO.
**PHQ/DAR/KIN/12336/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**YAH: MADAI YA TALAKA No. 2/2023**

**MADAI: AUDOKIA BONEPHACE**

**MDAIWA: ALCHERAUS APORINALI**

**KUITWA SHAURINI**

Ndugu **ALCHERAUS APORINALI** popote pale ulipo.
Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria tarehe 18/09/2023 bila kukosa.
Kama hautohudhuria basi shauri hili litasikilizwa upande mmoja na uamuzi utatolewa.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO BUGENE
RESIDENT MAGISTRATE
PRIMARY COURT
KARAGWE

## TANGAZO LA MNADA

Held auctioneer, EIE na Cops Auction Mart Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari na Nyumba jijini Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Unda Ramson Sigera | DAIHATSU T130DZU | 30.09.2023 |
| Johnson Jackson Mboje | TOYOTA RAV 4 T621 BAQ | 30.09.2023 |
| Jackson Jerome Mushi | TOYOTA PASSO T132 DDS | 30.09.2023 |
| Severin Otto Luambano | TOYOTA IST T910 DUB | 30.09.2023 |
| Rashda Hasani Msigiti | House Located at Gomba Muhimbili | 30.09.2023 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano piga**
**0655319097(cops),0657384471(EIE) au 0677014355(Fanikiwa) 0713197485(Held auctioneer)**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ERASTO CHARLES TINGATINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 202 DQY.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI
**PHQ/MBE/MBE/RB/1512/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**EDWARD PHILIP KOMOLO** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T 674 ARS, T 421 ASZ, T 492 BMF** zote aina ya MITSUBISHI FUSO. Yeyote atakayezione atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/ARU/ARU/2203/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Shija Felician Mlondela** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye Namba za usajili **T 119 DLL Toyota IST** yenye Chasis no. **NCP650009851** na Engine no. **INZ2459937.** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi.
RB Namba:
**PHQ/MWA/NYA/2398/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**HUSSEIN HAMISI MRISHO** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T 184 BFY, T 226 AAQ, T 698 AAA, T 220 CBE na T 848 BFW. Y**eyote atakayezione atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/ARU/MER/2261/2023.**

**OFISI ZA MATANGAZO,**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# 20,000 wahofiwa kufa kwa mafuriko Libya

**TRIPOL,** Libya

HOFU inazidi kutanda nchini Libya baada ya idadi ya waliokufa katika mafuriko yaliyolikumba eneo la Mashariki kufikia watu 20,000.

Meya wa mji wa Bandari wa Derna ambao umeharibiwa, alisema idadi hiyo ilitokana na wilaya zilizoharibiwa kabisa baada ya mabwawa mawili kupasuka na maji kuwasomba watu wakati wamelala.

Maji hayo yalipasua mabwawa hayo nyakati za usiku na hivyo watu wengi walishindwa kujiokoa.

Zaidi ya watu 5,300 hadi sasa wamethibitishwa kufariki dunia na wengine takribani 30,000 wakilazimika kuyahama makazi yao kutokana na mafuriko hayo.

**Serikali zote mbili zimewasiliana na jumuiya ya kimataifa kuomba huduma na usaidizi.**

Wafanyakazi wa misaada kutoka shirika la matibabu, Medecins Sans Frontieres, walitarajiwa kuwasili jijini jana,na kujiunga na timu za kukabiliana na dharura.

Miili mingi bado haijaopolewa chini ya vifusi au baharini, huku waokoaji wakiomba mifuko zaidi ya kuhifadhi miili ya watu.

Maelfu bado hawajulikani walipo huku waokoaji wakihangaika kufika eneo la Derna.

Wakati huo huo, serikali mbili zinazohasimiana nchini humo zinaratibu juhudi za kutoa msaada kwa waathirika wa mafuriko.

Ofisa wa Umoja wa Mataifa alisema kuwa serikali zote mbili za mashariki na magharibi zimeomba msaada wa kimataifa na zinawasiliana.

"Serikali zote mbili zimewasiliana na jumuiya ya kimataifa kuomba huduma na usaidizi," Tauhid Pasha, wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji, alikiambia kipindi cha The World Tonight cha BBC Radio 4.

"Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo inatawala magharibi imeomba msaada wetu na ombi lake kwa niaba ya nchi nzima na pia wanashirikiana na serikali ya mashariki," alisema.

"Changamoto sasa ni jumuiya ya kimataifa kujibu ipasavyo mahitaji na maombi ya serikali," aliongeza.

Pasha alisema msaada unahitajika kuongezwa haraka na inahitajika pesa kugharamia.

Tangu kuangushwa kwa mtawala wa muda mrefu Kanali Muammar Gaddafi mwaka 2011, Libya imegawanyika kati ya serikali mbili zinazohasimiana na kuingia katika mzozo kati ya wanamgambo.

Waziri Mkuu Abdul Hamid Dbeibah anaongoza Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa na Tripoli ni makao yake makuu.

Osama Hamad, waziri mkuu wa mashariki, anaongoza utawala hasimu unaojulikana kama Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo, wengi wanahisi nguvu inashikiliwa na jenerali hodari wa kijeshi Jenerali Khalifa Haftar, anayeongoza Jeshi la Kitaifa la Libya.

Jenerali Haftar alipokea ujumbe wa kijeshi wa Misri ambao ulikuja kutoa msaada baada ya maafa. **BBC**

## Tril. 11/- kutekeleza mradi kiuchumi Bagamoyo

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema Sh. trilioni 11 zinahitajika ili kutekeleza mradi mkubwa na wa kimkakati wa eneo maalum la kiuchumi la Bagamoyo. Ripoti ya upembuzi yakinifu na mpango kabambe wa utekelezaji wa mradi huo, imebainisha.

Ripoti hiyo iliwasilishwa katika mkutano wa Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, aliyeongoza timu ya maofisa kutoka wizarani kwake, Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), Kituo cha Uwekezaji Nchini (TIC), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na maofisa wengine kutoka wizara mbalimbali.

Katika kiwango hicho cha uwekezaji, serikali imepanga kutoa kiasi cha Sh. trilioni 1.6 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya msingi kama barabara, maji, umeme na gesi asilia.

Prof. Mkumbo alisema uhuishaji wa mradi wa Bagamoyo unatokana na uamuzi wa msingi uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kutaka mradi huo utekelezwe baada ya kukwama kwa zaidi ya miaka 10.

"Kutokana na taarifa iliyopo katika ripoti iliyowasilishwa, inakadiriwa kuwa kiasi cha Sh. trilioni 11 zitahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu mkubwa na wa kimkakati kwa manufaa ya nchi yetu," alisema.

Alisema katika mradi huu, zaidi ya viwanda 200 vinatarajiwa kujengwa ambavyo vitachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi na ajira nchini.

Mradi wa Bagamoyo utakuwa na maeneo 19 ikijumuisha ya viwanda, biashara na huduma. Kwa mfano kutakuwa na maeneo ya viwanda na biashara huru pamoja na bandari.

Prof. Mkumbo alisema mradi wa Bagamoyo ulipangwa kuwa wa pili baada ya wa Benjamin Mkapa uliopo eneo la Mabibo External, jijini Dar es Salaam.

Prof. Mkumbo, alisema baada ya uamuzi wa Rais Samia mambo yameanza tena kwa kasi katika kuutekeleza mradi huo.

Alisema hadi sasa hekta 5,473 zimepimwa kati ya 9,800 za eneo lote na hekta 2,422 zimeshalipiwa fidia huku 3,320 zikibaki.



Wafanyakazi wa uokoaji wakiendelea kutafuta miili ya watu katika mji wa Derna nchini Libya baada ya mafuriko kusababisha vifo zaidi ya 5000. **PICHA: AFP**

## Shule yachunguzwa tuhuma za udanganyifu Mtihani Darasa VII

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo, mkoani Pwani, Shauri Selenda, amesema wanafanya uchunguzi dhidi ya shule moja ya msingi wilayani mwake, inayotuhumiwa kufanya udanganyifu katika Mtihani wa Taifa wa Darasa la VII uliofanyika kwa siku mbili; juzi na jana nchini.

Katika mazungumzo na Nipashe ofisini kwake mjini Bagamoyo juzi, Selenda alisema amepokea taarifa za baadhi ya maofisa wake kuhusishwa na hujuma dhidi ya mtihani huo katika moja ya shule za msingi (siyo ya serikali) wilayani mwake.

Alibainisha kuwa walichukua hatua za kuwaengua katika usimamizi wa mtihani huo maofisa hao ili kupisha uchunguzi kutokana na kutuhumiwa kujihusisha na jinai hiyo.

"Taarifa hizi zimetufikia na tayari tumeanza kuzifanyia kazi kwa kuwaweka pembeni katika suala zima la usimamizi wa mitihani na tumeunda timu ya uchunguzi kama wilaya tuone kama waliotajwa wanahusika ili hatua za kisheria zichukuliwe.

"Kutokana na tuhuma hizi, kama wilaya tumeimarisha ulinzi katika vituo vyote vya kufanyia mitihani, hivyo ninapenda kuwatoa hofu wananchi wasiwe na wasiwasi kuhusu suala hilo," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema taarifa hiyo inaonyesha kuwa mbali ya waliotajwa, kuna mtandao mkubwa unaohusisha watu wengi kuanzia Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) hadi Wizara ya Elimu, hivyo uchunguzi huo utaendelea kwa ngazi zote.

Ofisa Uhusiano wa NECTA, John Nchimbi, alisema taarifa hizo wamezipokea na wanazifanyia kazi.

"Ndugu mwandishi, taarifa hizi tumezipokea na tutazifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili tubaini ukweli wa jambo hilo. Ikibainika, kila aliyehusika atachukuliwa hatua za kisheria," alihadharisha.

Katika baadhi ya mitandao ya kijamii mwanzoni mwa wiki, kulikuwa na taarifa inayodaiwa kutumwa wizarani na baadhi ya walimu wanaojiita 'wazalendo' katika shule hiyo, wakidai Mratibu Elimu Kata, baadhi ya maofisa wanaohusika na elimu wilayani Bagamoyo, pia baadhi ya maofisa wa NECTA wamefanya hujuma za mtihani huo katika shule hiyo.

Mwandishi alipomtafuta meneja wa shule hiyo (jina tunalihifadhi kutokana na sababu za kiuchunguzi na kisheria) kuzungumzia suala hilo, alisema "vyombo vya usalama vinafanya uchunguzi. Sina cha kusema zaidi kwa sasa".



MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

# Mfanyakazi wa ndani atoa ushahidi kesi mauaji dada wa Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

MFANYAKAZI wa ndani wa Aneth Msuya, Getruda Mfuru (38), jana alitoa ushahidi katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, akieleza washtakiwa walivyofika nyumbani kwa marehemu Aneth kabla ya kutekeleza mauaji hayo.

Mfuru ambaye ni shahidi wa 25, aliongozwa na Wakili wa Jamhuri, Paul Kimweri, alitoa ushahidi kuhusiana na mauaji ya Aneth Msuya, dada wa Bilionea Msuya, yaliyotokea Mei 26, 2016 Kibada, Kigamboni mkoani Dar es Salaam na ifuatayo ni sehemu ya ushahidi huo;-

**Kimweri: Tukumbushe jina lako.**

**Shahidi:** Naitwa Getruda Peniel Mfuru mzaliwa wa Kijiji cha Masama, Sonu, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

**Kimweri: Hebu ieleze mahakama unajishughulisha na nini? Pia ueleze kuhusu familia yako na elimu yako kwa ufupi.**

**Shahidi:** Najihusisha na kilimo cha mboga na ufugaji wa kuku na mbuzi. Familia yangu tumezaliwa watatu na mimi ni wa pili kuzaliwa. Elimu yangu ni kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Olorieni, Arusha mwaka 2005.

**Kimweri: Baada ya kumaliza kidato cha nne nini kiliendelea.**

**Shahidi:** Baada ya kumaliza kidato cha nne nilikosa uwezo wa kuendelea na shule ikabidi nirudi kwa bibi kwa sababu baba na mama walikuwa wamefarakana.

**Kimweri: Hebu ieleze mahakama maisha yalivyoendelea huko kijijini kwa bibi yako. Ilipofika mwaka 2007 nini kilitokea?**

**Shahidi:** Nikiwa kwa bibi mwaka 2007 nilipata mtoto wangu wa kwanza wakafuata na watoto wengine wawili mwaka 2019 na 2013. Kwa sasa ni mama wa watoto wawili mmoja marehemu.

**Kimweri: Ilipofika mwaka 2015 nini kiliendelea?**

**Shahidi:** Ilipofika mwaka 2015 niliamua kutafuta kazi za ndani. Katika kutafuta nilikutana na mama Manka, nikamueleza akaniambia kuna mama anaitwa Bibi Msuya anaishi Cairo, Mererani anahitaji dada wa kazi.

**Kimweri: Baada ya hapo ilifuata hatua gani?**

**Shahidi:** Mama Manka aliniunganisha na yule bibi Msuya na Bibi Msuya alinipigia simu.

**Kimweri: Baada ya bibi Msuya kukupigia simu nini kilifuata?**

**Shahidi:** Bibi Msuya alinitumia Sh 10,000 kwa njia ya MPESA kwa ajili ya nauli ya kwenda Cairo Mererani. Baada ya kunitumia fedha nilikwenda huko.

**Kimweri: Ieleze mahakama ilikuwa mwezi gani na mwaka gani ulisafiri kwenda Cairo Mererani?**

**Shahidi:** Ilikuwa Februari 15, 2015.

**Kimweri: Baada ya kufika mliingia makubaliano gani?**

**Shahidi:** Baada ya kufika kwa Bibi Msuya tulikubaliana kwamba atakuwa ananilipa Sh. 40, 000 kwa mwezi na hapo nyumbani kwake kulikuwa na wafanyakazi wengine watatu wa kike.

**Kimweri: Kwa Bibi Msuya ulifanya kazi hadi lini?**

**Shahidi:** Nilifanya kazi hadi Agosti 28, 2015. Ilipofika tarehe hiyo nilimwambia Bibi Msuya kuwa nataka kwenda nyumbani kwa ajili ya kuangalia watoto wangu, akanijibu sawa.

Peter Kibatala (wakili wa utetezi): Samahani Mheshimiwa Jaji, shahidi kuna sehemu anasoma maana hatumuelewi.

**Shahidi:** Huku akijigeuza mwili wake na kunyoosha mikono juu, alimweleza jaji kwamba hasomi sehemu yoyote.

**Kibatala:** Mbona kama anasoma mheshimiwa jaji.

**Jaji:** Unaweza kwenda kujiridhisha.

**Kibatala:** Akatoka alipokaa na kuanza kusogea kwenye kizimba cha shahidi. Shahidi alitoka kwenye kizimba huku akinyoosha mikono juu kuwa hakuna anachosoma.

Kibatala alichungulia ndani ya kizimba na hakuona sehemu yoyote ambayo shahidi alikuwa anasoma.

**Kimweri: Kwa kipindi chote ulichokaa kwa Bibi Msuya ulifanikiwa kumfahamu nani?**

**Shahidi:** Katika kipindi chote nilichoishi pale kwa Bibi Msuya nimewahi kuwafahamu na kuwaona watoto wake wanne, Dada Antuja, Dada Bahati, Dada Joyce na Dada Aneth.

**Kimweri: Maisha baada ya kurudi kijijini kwa bibi ilipofika Desemba 24,2015 nini kilitokea?**

**Shahidi:** Niliishi na bibi yangu hadi Desemba 24,2015 nilipopata simu kutoka kwa Bibi Msuya akinieleza kwamba mtoto wake anayeishi Dar es Salaam (Aneth) anahitaji dada wa kazi. Nilimwambia naweza kwenda.

**Kimweri: Baada ya Bibi Msuya kukuunganisha na Aneth kwenye mawasiliano ya simu nini kiliendelea?**

**Shahidi:** Aneth alinipigia simu nikazungumza naye na kunitumia Sh 22,000.

**Kimweri: Hizo fedha alizokutumia ulizifanyia nini?**

**Shahidi:** Nilichukua Sh. 10,000 nikampa bibi na nyingine 10,000 nilifanya nauli ya kwenda Cairo Mererani kwa Bibi Msuya Desemba 25,2015 na hiyo elfu mbili ilikuwa ya kutolea.

**Kimweri: Baada ya kufika kwa Bibi Msuya nini kiliendelea?**

**Shahidi:** Nilikaa pale hadi Januari 4, 2016. Tarehe hiyo niliondoka na Antuja kwenda Dar es Salaam kwa Aneth Msuya, tulienda Kigamboni.

**Kimweri: Nini sasa kiliendelea baada ya kufika kwa Aneth?**

**Shahidi:** Aneth alinielekeza majukumu ya kazi na mshahara ambao tulikubaliana kuwa atanilipa Sh. 60, 000 kila mwezi. Aliahidi kuwa hadi Juni, 2016 ataniongezea mshahara kwa kuwa ile familia ya Aneth ilikuwa na watu watatu, Aneth Msuya, Allan na mtoto wa Aneth.

Katika kipindi chote nilichokaa pale, sikuwahi kumwona rafiki au mume wa Dada Aneth. Aliishia kunionesha mume wake kwenye picha. Hali ya maisha na uhusiano na Aneth yalikuwa maisha yenye furaha na amani. Pia mahusiano ya Aneth na watu wengine, yaani majirani, yalikuwa mazuri na walikuwa wanaishi vizuri na kwa amani kabisa.

Ilipofika Mei 5, 2016 majira ya mchana, nilikuwa nyumbani na Aneth, nilitokea geti la nyuma kwa ajili ya kwenda kununua 'toilet paper' dukani.

Nikiwa njiani nilikutana na gari la 'dark blue' kilishushwa kioo cha nyuma cha gari na baada ya kioo kushushwa, nilimuona mama aliyevaa suti rangi ya bluu, singlendi nyeusi, cheni mbili moja kubwa moja nyembamba, zilikuwa na mwonekano wa dhahabu, ana uso wa mviringo na amesuka nywele za kitimtimu na hereni alivaa.

Baada ya hapo alinimbia samahani naomba kuongea na wewe ndipo nilipomfuata pale alipokuwa na kule ndani ya gari niligundua kuna mtu mwingine wa kiume ambaye alikuwa upande wa dereva wa hilo gari.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya hapo yule mwanamke alimuuliza kama anapajua kwa Aneth Msuya na kumjibu ndiyo. Baada ya hapo, alimwonyesha kwa ishara na kumweleza kuwa naye ni dada yake.

Alidai kuwa yule mwanamke alimwambia msichana wa kazi kuwa wataonana kesho. Hata hivyo, alidai kuwa yule mwanamke hakufika siku hiyo ambayo ilikuwa Mei 17, 2016. Wakati wanakutana na yule mwanamke, alidai kuwa Aneth alikuwa kazini.

Mfuru alidai kuwa Mei 18, 2016 majira ya saa 4:00 asubuhi alikuwa nyumbani. Wakati anatoka kwenda kuchota maji, akamkuta yule mwanamke amefuatana na yule mwanamume aliyekuwa naye kwenye gari alilokutana nalo siku ile nje ya geti.

Alidai kuwa siku hiyo mwanamke huyo alikuwa amevaa suti ya cream na viatu vya zambarau na cheni kubwa mbili za muonekano wa dhahabu, moja pana na nyingine nyembamba na hereni kichwani amesukia 'weaving'.

"Hii suti ilikuwa sketi fupi na miguu yake haikuwa minene ila juu alikuwa mnene. Mwanamume aliyekuwa naye alikuwa amevaa suti nyeusi, shati jekundu na viatu vyeupe, alikuwa amevaa miwani ameipandisha kwa juu kichwani. Alikuwa mrefu saizi na mnene saizi na mweusi," alidai.

Baada ya yule mwanamke kumwita, alidai kuwa ilibidi arudishe ndoo ndani ya geti ndio akawafuata na kuwakuta wameshaingia kwenye gari. Gari hilo, alidai lilikuwa la kifahari Range Rover rangi ya silver.

Alidai kuwa alipofika kwenye gari, yule mwanamke alimtaka aingie na akaingia kwenye gari na kuwakuta watu wanne na yeye akawa wanne. Huyo mtu mwingine alikuwa mwanamume amevaa tisheti nyekundu na suruali ya jeans ya bluu. Baada ya kuingia kwenye gari yule mama akachukua pochi yake akatoa simu aina ya Nokia ndogo na akampa kisha akamwambia "shika hii simu tutakuwa na mawasiliano ya mara kwa mara mimi na wewe."

Pia alidai kuwa mwanamke yule alimwambia asiwasiliane na mtu mwingine yeyote na wakijua anawasiliana na mtu mwingine watamwadabisha. Alidai wakati akiwa ndani ya gari, yule mwanamke alikuwa anamwambia dereva "mali nitafute mimi na mume wangu wengine wanazihangaikia za nini na yule mwanamume akajibu kwa kuguna mmh hao ni wapumbavu tu."

Akiwa bado ndani ya gari aligeukia mama na kumwambia hii simu ni ya nini? alimjibu hiyo simu watakuwa wanawasiliana na yeye mara kwa mara. Aliendelea kueleza kuwa yule kaka ambaye alikuwa amevaa tisheti nyekundu alitoa bastola na kumwekea shingoni mara tu baada ya kumuuliza yule mama hiyo simu ya nini.

Kutokana na hali hiyo, alidai kuwa alijisikia vibaya na kupata hofu kubwa sana. Hiyo simu aliyopewa ilikuwa na mtandao wa Airtel na namba zake hakuzishika kichwani. Alidai kabla ya kuachana nao na wakati anakabidhiwa simu walimweleza kuwa wana kazi na dada Aneth na alipomwuliza ni kazi gani, alimjibu kuwa haimhusu.

Baada ya kuweka bastola waliendelea kuongea kilugha ambacho yeye hakuwahi kukijua. Baada ya kuondoka na kwenda nyumbani, alizima ile simu na kuchukua hatua ya kuficha kwenye kochi dogo ambalo lilikuwa halitumiki.

Alidai kuwa aliamua kuzima simu hiyo ili Aneth asisikie akiwa anawasiliana na mtu mwingine. Baada ya kuzima simu, alidai kuwa kesho yake dada aliondoka kwenda kazini yeye aliiwasha.

Pia alidai kuwa hakumweleza Aneth chochote kuhusu matukio hayo kutokana na vitisho alivyopewa. Mei 23, 2016 akiwa nyumbani. Alidai alipigiwa simu na yule mama kwa kutumia simu aliyompa akamwambia waonane nje.

"Nilitoka na niliwakuta mbele ya nyumba, aliwaomba wasogee kidogo kwa kutumia gari aina ya Range Rover rangi la silver. Alipofika aliegemea gari na yule mama aliniambia ingia ndani ya gari," alidai Mfuru.



Mshtakiwa wa kesi ya mauaji ya dada wa marehemu Bilionea Msuya, Miriam Mrita akiwa chini ya ulinzi wa askari magereza baada ya kufikishwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam juzi, kusikiliza kesi inayomkabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

ZISIKUPITE

## TONEY ATAKIWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inamtaka mshambuliaji wa Brentford ya England, Ivan Toney, 27, ambaye anatumikia marufuku ya miezi nane kwa kukiuka sheria za kamari. Mchezaji huyo haruhusiwi kucheza hadi Januari 17 2024, lakini anaweza kurejea mazoezini wikendi hii. ***(football.london)***

## PARTEY KUMRITHI POGBA

JUVENTUS inampanga kiungo wa kati wa Arsenal na Ghana, Thomas Partey, 30, kama mbadala wa kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye miaka 30, ambaye mkataba wake unaweza kusitishwa ikiwa atabainika kukiuka sheria za kupinga matumizi ya dawa za kusisimua misuli. ***(La Repubblica)***

## HARRY ALIKARIBIA WEST HAM

MLINZI wa Manchester United na England, Harry Maguire, 30, alikuwa "karibu sana" kujiunga na West Ham kwa mkataba wa pauni milioni 30 msimu huu, amesema kocha wa wagonga nyundo hao, Kevin Nolan. ***(Sport)***

## MO SALAH ATAONDOKA

MLINZI wa zamani wa Liverpool na England, Glen Johnson amesema hatashangaa iwapo Mohamed Salah, 31, ataondoka Anfield na kuelekea Saudi Arabia. Liverpool ilikataa dau la pauni milioni 150 kutoka kwa klabu ya Al-Ittihad mwezi huu. ***(Liverpool Echo)***

## SHELVEY KUTUA UTURUKI

KIUNGO wa kati wa zamani wa Nottingham Forest na England, Jonjo Shelvey, 31, anakaribia kujiunga na klabu ya Uturuki ya Rizespor kabla ya leo Ijumaa. Shelvey alijiunga na Forest kutoka Newcastle United kwa mkataba wa miaka miwili na nusu mwishoni mwa Januari. Wakati huo huo, fowadi wa Forest na Nigeria, Emmanuel Dennis, 25, pia anakaribia kuondoka katika klabu hiyo. ***(Telegraph)***

## KLOPP AMEKATAA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, 56, amekataa kuwa kocha wa Ujerumani kufuatia kutimuliwa kwa Hansi Flick. Mjerumani Klopp amekuwa Anfield tangu mwaka 2015. ***(Sportschau)***

## BEEK AGOMBEWA

KLABU za nchini Uturuki na Qatar vinapigiwa upatu huku Manchester United ikitafuta kumuuza kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, 26. Hata hivyo, sasa inaonekana huenda mchezaji huyo wa zamani wa Ajax atasalia Old Trafford hadi Januari. ***(Sun)***

## MEJBRI ANASAKWA

KIUNGO wa kati wa Manchester United na Uturuki, Hannibal Mejbri, 20, anasakwa kwa mkopo na Besiktas. Dirisha la uhamisho nchini Uturuki linafungwa leo Ijumaa. ***(Mirror)***

## HAZARD KUSTAAFU

WINGA wa zamani wa Chelsea na Ubelgiji, Eden Hazard anafikiria kustaafu akiwa na umri wa miaka 32 baada ya kuachwa na Real Madrid. ***(CaughtOffside)***

## POTTER AMEKATAA

BOSI wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter, 48, ameripotiwa kukataa kuifundisha Lyon ya Ufaransa na Rangers ya Scotland. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PARTEY ATAJWA KURITHI MIKOBA YA POGBA JUVE

### ●●● Ni kutokana na hofu ya Mfaransa huyo kugundulika kutumia dawa za...

**TURIN,** Italia

HOFU iliyotokana na tukio la Paul Pogba kugundulika kutumia dawa ya kusisimua misuli imesababisha Mkurugenzi wa michezo wa Juventus, Cristiano Giuntoli kutafuta viungo wa kuziba pengo.

**Kwa mujibu wa mtandao wa michezo Calciomercato wa Italia, miamba hiyo ya Serie A imeorodhesha wachezaji kadhaa inaoona wanafaa kuchukua nafasi hiyo.**

Kiungo wa 'Washika bunduki' wa London, Arsenal, Thomas Partey anapewa nafasi ya kwanza katika orodha hiyo, huku wakiripotiwa kuwa tayari kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kuondoka pale Emirates.

Khephren Thuram wa Nice ni mchezaji mwingine ambaye Giuntoli anaona kivutio, lakini pia anaweza kuwa ghali zaidi kwenye orodha hiyo kwa kuwa na thamani ya euro milioni 35.

Juve pia inasaka saini ya Manu Kone wa Borussia Monchengladbach, ambaye awali aliwasiliana na AC Milan wakati akikiwasha Toulouse ya Ufaransa na amekuwa katika kiwango bora tangu alipohamia Bundesliga.

Kiungo wa Strasbourg, Habib Diarra ndiye anayefuata katika orodha hiyo, lakini Juve inaweza kukabiliwa na ushindani mkubwa kutoka Wolfsburg katika kumsajili kiungo huyo mwenye umri wa miaka 19 anayekadiriwa kuwa na thamani ya Euro milioni 20.

Mchezaji wa mwisho katika orodha hiyo ni Abdoulaye Kamara kutoka Borussia Dortmund, ingawa Juve inataka kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 18 kama tegemeo la baadaye kuliko wa kikosi cha kwanza kwa sasa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,152,9

MECHI KALI
BAYERN MUNCHEN
VERSUS
BAYER LEVERKUSEN
1 | 1.65
X | 4.49
2 | 4.49

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Chacha Chacha - 0652 042 XXX
2. Dulla Nice - 0653 950 XXX
3. Suzana Mwahasunga - 0656 788 XXX
4. Luckson Simon - 0656 900 XXX
5. Abasi Kiloko - 0657 109 XXX
6. Haruna Omari - 0672 760 XXX
7. Yeremia Daudi - 0673 110 XXX
8. Hamza Saidi - 0676 303 XXX
9. Mohamed Njiwa - 0676 742 XXX
10. France Msoma - 0679 621 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VERRATTI ATIMKIA AL ARABI YA QATAR



**DOHA,** Qatar

KIUNGO wa kati wa Italia, Marco Verratti, ameondoka Paris Saint-Germain na kujiunga na klabu ya Qatar, Al Arabi, kwa mujibu wa ESPN.

Verratti amesaini mkataba wa miaka mitatu na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Qatar ambayo imelipa kiasi cha Euro milioni 45 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

"Nilijivunia sana kuvaa rangi za Paris St. Germain kwa zaidi ya muongo mmoja, kusugua mabega na wachezaji wengi wazuri, na kushinda mataji 30," alisema Verratti akiiambia tovuti ya PSG.

"Paris, Klabu na wafuasi wake daima watakuwa na nafasi ya pekee sana moyoni mwangu."

Verratti, ambaye hajawahi kucheza Serie A ya Italia, alijiunga na PSG mwaka 2012 akitokea klabu ya Pescara ya kwao. Timu hiyo ya Ligue 1 ililipa euro milioni 12 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 wakati huo.

Katika misimu 11 akiwa PSG, Verratti alicheza katika mechi 416, na kumfanya kuwa mchezaji wa pili kwa kucheza mechi nyingi zaidi katika klabu hiyo baada ya Jean-Marc Pilorget (435).

Aliisaidia PSG kushinda mataji tisa ya ligi, na kushinda 'Coupe de France' na 'Coupe de la Ligue' mara sita.



## PSG yataka wa5 Real kulipiza kisasi

**PARIS,** Ufaransa

TIMU ya Paris Saint-Germain (PSG), imeripotiwa kuandaa orodha ya wachezaji wa Real Madrid 'Los Blancos' ili kuwasajili kulipiza kisasi cha klabu hiyo ya Hispania kila mara kuonesha nia kwa Kylian Mbappe.

Nia inayoendelea ya Real Madrid kwa nyota huyo wa Ufaransa imeleta misukosuko kwa mabingwa hao wa Ligue 1, na Mbappe anaonekana anakusudia kwenda Bernabeu majira yajayo ya kiangazi.

Kwa mujibu wa tovuti ya michezo, Sport, sasa PSG inapanga kuvamia vito vya Madrid kujibu mashambulizi, huku Rais wa PSG Nasser Al-Khelaifi akionekana ana nia kusajili wachezaji watano.

Wachezaji hao ni Vinicius Jr, Rodrygo, Aurelien Tchouameni, Eduardo Camavinga na Federico Valverde.

Kikwazo kikubwa katika mpango huo ni vifungu vikubwa vya kuachiwa ambavyo klabu za Hispania zimekuwa zikiwawekea wachezaji wao wenye vipaji.

Vinicius Jr ameripotiwa kusaini mkataba mpya majira ya kiangazi wenye kifungu cha kuachiwa cha pauni milioni 860 sawa na shilingi trilioni 2.6 na Madrid mara chache hupoteza wachezaji wenye vipaji kwenda klabu nyingine.

911,993/-



# VIBONDE WA YANGA SC WATUNISHIANA MISULI

Na Mwandishi Wetu

KUFUATIA kuwepo kwa mazingira mazuri yaliyowekwa na Mkuu wa Majeshi Jenarali Jacob Mkunda, katika kuendeleza michezo na kufikia malengo ya kupeleka timu yake kwenye michuano ya kimataifa, uongozi wa klabu ya Mashujaa FC ya Kigoma umejipanga na kudhamiria kufikia malengo hayo.

**Katika kuhakikisha wanafikia malengo ya kumaliza ligi wakiwa miongoni mwa klabu za 'Top Four', benchi la ufundi la timu hiyo limedhamiria kufanya vizuri kwenye michezo yake yote na watahendelea kusaka pointi tatu kwenye mchezo wa kesho dhidi ya Ihefu FC utakaochezwa Mbarali mkoani Mbeya.**

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Meja IY Mgaya, alisema Mkuu wa Majeshi ameweka mazingira mazuri ambayo yanatoa nafasi kwa timu kupambana na kufikia malengo yao.

Alisema Mashujaa FC imekuwa ikiishi kwenye mazingira mazuri tangu kupanda kwenye ligi na inasafiri kwa wakati kufika kwenye mkoa kucheza michezo yao ya ligi kuu.

"Tunataka kuhakikisha tunapata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa kwa kumaliza katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu kutokana na mazingira mazuri ambayo afande CDF ameyaweka kwa timu zetu," alisema Meja Mgaya.

Aidha, alisema uwepo wa mashabiki wenye 'Mzuka' mkoani Kigoma anaamini uwanja wao wa Mashujaa mkoani humo utakuwa machinjio ya timu pinzani.

"Tuna mchezo dhidi ya Ihefu, naamini tutafanya vizuri na kuondoka na pointi zote tatu muhimu na kuendelea kuwa kwenye nafasi nzuri," alisema Meja Mgaya.

Kuelekea mchezo huo wa kesho utakaochezwa uwanja wa Mashujaa mkoani Kigoma, kocha wa timu hiyo, Mohamed Abdallah 'Bares' amesema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kuondoka na pointi tatu.

"Tunafahamu tutacheza nyumbani, tumejipanga na tunaendelea kujiimarisha, tunataka kupata pointi tatu muhimu na hilo linawezekana," alisema Bares.

Kocha huyo ameweka wazi namna wachezaji wake walivyojiandaa na kuwa na shauku ya mchezo huo.

"Mchezo huu ni muhimu sana kwetu, lengo letu ni pointi tatu, tunashukuru namna ambavyo wachezaji wetu wanapambana na kuwa na utayari muda wote, tunaamini tutafanya vizuri kwenye mchezo huu na michezo mingine mbele yetu," alisema Bares.

Timu hiyo iliyopanda Ligi Kuu kwa kishindo msimu huu, inamilikiwa na Jeshi la Wananchi (JWTZ) chini ya uratibu wa karibu na Kurugenzi ya Michezo na utimamu wa mwili inayoongozwa na Martin Msumari.

Kwa muda mrefu sasa Jeshi la Wananchi limekuwa na mchango mkubwa kwenye kukuza soka hapa nchini ambapo wamekuwa wakiwapa nafasi vijana wenye vipaji kujiunga na timu zao.

Aidha, wamekuwa wakisaidia kukuza soka la vijana na kuwa mdau mkubwa wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Mashujaa FC ilipanda daraja msimu huu baada ya kufanikiwa kuibuka na ushindi wa jumla kwenye mchezo wa 'Play Off' dhidi ya Mbeya City kwa ujumla ya ushindi wa mabao 4-1.

Mpaka sasa Mashujaa FC inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi ikiwa na pointi nne nyuma ya vinara, Yanga, Azam na Simba wenye pointi sita baada ya timu zote kucheza michezo miwili.

Mashujaa ilianza kwa ushindi mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu kwa kuifunga Kagera Sugar kwa bao 1-0 kabla ya kutoshana nguvu na Geita Gold FC kwenye mchezo wake wa pili.

## Gamondi awafungia kazi nyota nane

INATOKA UK. 24

nilishawaona kwenye baadhi ya video za klabu yao.., kama benchi la ufundi kwa kiasi kikubwa kazi yetu tumeifanya, kazi imebaki kwa wachezaji wetu ambao nina imani nao sana kutupa matokeo mazuri," alisema Gamondi.

Alisema Al Merrikh ni timu kubwa na ina wachezaji wazuri ambao itawafanya wao (Yanga) kucheza kwa tahadhari kwenye mchezo huo wa ugenini.

"Ni jambo zuri sana kama timu kuona tutakuwa na mashabiki wetu wa kutosha uwanjani, hii itatupa hamasa sana, kwa kweli wachezaji wanajivunia kuwa na mashabiki wa aina hii," alisema Gamondi.

**Msafara wa mashabiki kutua Kigali**

Jana yalionekana magari ya mashabiki yakianza safari kuelekea Kigali kuishangilia timu yao kwenye mchezo huo muhimu.



Wachezaji wa timu ya Kitunda FC, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Robertinho awashika pabaya*

INATOKA UKURASA 24

njiani kama sisi kwenda kuwapa hamasa wachezaji wetu," alisema Ahmed akiwa njiani kuelekea nchini humo.

Baada ya mechi hiyo ya mkondo wa kwanza, Simba inatarajiwa kuwa mwenyeji katika mechi ya marudiano, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Septemba 29.

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.16/09/23 | 17:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.41 | 3.25 | 2.80 |
| 02.16/09/23 | 17:00 | Kilmarnock FC vs Hibernian FC | 2.48 | 3.30 | 2.70 |
| 03. 16/09/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs FC Famalicao | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 04. 16/09/23 | 19:00 | Inter Milano vs AC Milan | 2.16 | 3.35 | 3.15 |
| 05. 16/09/23 | 19:30 | VfL Bochum vs Eintracht Frankfurt | 2.80 | 3.50 | 2.27 |
| 06. 16/09/23 | 20:00 | USL Dunkerque vs Grenoble Foot | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 07. 16/09/23 | 20:00 | Rodez Aveyron Football vs Angers SCO | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 16/09/23 | 20:00 | Paris FC vs Amiens SC | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 16/09/23 | 20:30 | SK Sturm Graz vs FC Salzburg | 2.70 | 3.30 | 2.24 |
| 10. 16/09/23 | 21:45 | Cardiff City vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 17/09/23 | 13:30 | Cagliari Calcio vs Udinese Calcio | 2.85 | 3.25 | 2.39 |
| 12. 17/09/23 | 15:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.50 | 2.90 | 2.95 |
| 13. 17/09/23 | 15:30 | FC Twente Enschede vs Ajax Amsterdam | 2.65 | 3.35 | 2.48 |
| 14. 17/09/23 | 16:00 | Frosinone Calcio vs Sassuolo Calcio | 2.75 | 3.35 | 2.40 |
| 15. 17/09/23 | 16:30 | FC Heidenheim vs Werder Bremen | 2.27 | 3.70 | 2.70 |
| 16. 17/09/23 | 17:15 | US Catanzaro vs Parma Calcio | 2.42 | 3.00 | 2.65 |
| 17. 17/09/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs Atalanta BC | 2.35 | 3.45 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 15/09/2023


| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1470 | Kawasaki Frontale vs FC Tokyo | 1.87 | 3.48 | 3.48 |
| 13:00 | 3987 | Yokohama F Marinos vs Sagan Tosu | 1.44 | 4.57 | 5.07 |
| 13:30 | 4708 | Urawa Red Diamonds vs Kyoto Sanga | 1.64 | 3.50 | 4.66 |
| 16:00 | 2889 | Bangkok Utd vs Sukhothai FC | 1.38 | 4.46 | 6.28 |
| 18:00 | 1306 | AL Faiha vs Al Shabab Riyadh | 3.34 | 3.60 | 2.03 |
| 18:00 | 5379 | El Bayadh vs CS Constantine | 2.11 | 3.10 | 3.31 |
| 18:30 | 3733 | Opava vs Dukla Prague | 2.58 | 3.23 | 2.42 |
| 18:30 | 5841 | FC Metalist 1925 vs Zorya Lugansk | 4.15 | 3.39 | 1.74 |
| 18:45 | 4436 | AL Qaisoma vs AL Ain | 2.43 | 2.95 | 2.70 |
| 18:45 | 4986 | AL Khlood vs AL Jandal | 1.93 | 3.13 | 3.68 |
| 19:00 | 1197 | Dodoma FC vs Mtibwa Sugar | 2.00 | 3.20 | 3.75 |
| 19:00 | 3162 | Dinamo Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.62 | 3.75 | 4.83 |
| 20:00 | 4084 | Viborg FF vs Midtjylland | 2.82 | 3.37 | 2.36 |
| 20:00 | 5946 | Ranheim vs Raufoss | 2.36 | 3.44 | 2.53 |
| 20:30 | 3274 | FC Wil vs FC Stade LS Ouchy | 2.25 | 3.74 | 2.51 |
| 20:30 | 5028 | Neuchatel Xamax vs BSC Young Boys | 6.06 | 4.85 | 1.35 |
| 20:30 | 5209 | Moroka Swallows FC vs Richards Bay FC | 2.05 | 3.04 | 3.66 |
| 21:00 | 1144 | Jong Ajax vs Emmen | 3.27 | 3.79 | 1.90 |
| 21:00 | 1838 | Al Hilal Riyadh vs AL Riyadh | 1.11 | 8.36 | 20.90 |
| 21:00 | 2072 | Groningen vs ADO Den Haag | 1.59 | 3.89 | 4.81 |
| 21:00 | 2141 | Al Ahly Cairo vs USM Alger | 1.66 | 3.36 | 4.99 |
| 21:00 | 2340 | Jong PSV vs De Graafschap | 2.86 | 3.57 | 2.15 |
| 21:00 | 3180 | ASO Chlef vs MC Oran | 1.59 | 3.35 | 5.20 |
| 21:00 | 3283 | VVV Venlo vs NAC Breda | 2.54 | 3.48 | 2.42 |
| 21:00 | 3526 | Helmond Sport vs FC Oss | 1.70 | 3.68 | 4.29 |
| 21:00 | 3854 | Jong AZ Alkmaar vs FC Eindhoven | 2.25 | 3.38 | 2.82 |
| 21:00 | 4133 | Al Khaleej Club vs Al Fateh (KSA) | 3.08 | 3.55 | 2.16 |
| 21:00 | 4334 | Soroksar vs Kecskemeti TE | 4.59 | 3.72 | 1.63 |
| 21:00 | 4354 | Dordrecht vs Jong Utrecht | 1.84 | 3.58 | 3.68 |
| 21:00 | 4863 | Roda Kerkrade vs Telstar | 1.77 | 3.68 | 3.88 |
| 21:00 | 5660 | Den Bosch vs Maastricht | 2.14 | 3.52 | 2.91 |
| 21:15 | 2957 | CF Estrela vs Porto | 7.57 | 4.78 | 1.34 |
| 21:30 | 2970 | Bayern Munchen vs Bayer Leverkusen | 1.65 | 4.49 | 4.49 |
| 21:30 | 3124 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.41 | 3.63 | 2.39 |
| 21:30 | 5390 | Venezia vs Spezia | 2.28 | 3.29 | 2.88 |
| 21:45 | 1043 | Derry City vs Shamrock Rovers | 2.27 | 3.08 | 2.89 |
| 21:45 | 1749 | Larne vs Linfield Belfast | 2.13 | 3.23 | 3.03 |
| 21:45 | 2112 | Galway United vs Dundalk FC | 2.69 | 3.35 | 2.33 |
| 21:45 | 2583 | Cork City vs Wexford Youths | 1.28 | 4.88 | 8.74 |
| 21:45 | 3382 | Hull City vs Coventry | 2.67 | 3.26 | 2.45 |
| 21:45 | 3413 | KVC Westerlo vs Royal Antwerp | 4.47 | 3.77 | 1.68 |
| 21:45 | 3431 | Colwyn Bay vs Aberystwyth Town | 2.09 | 3.38 | 2.98 |
| 21:45 | 5535 | Drogheda Utd vs Bohemians FC | 2.81 | 3.37 | 2.24 |
| 22:00 | 1832 | Paris St Germain vs Nice | 1.56 | 4.36 | 5.63 |
| 22:00 | 3090 | Rayo Vallecano vs Alaves | 1.94 | 3.24 | 4.42 |
| 22:00 | 3470 | Southampton vs Leicester | 2.29 | 3.42 | 2.77 |
| 22:00 | 5470 | Finn Harps vs St Patricks | 11.16 | 5.48 | 1.21 |
| 22:15 | 2370 | Pacos Ferreira vs Leixoes | 1.59 | 3.69 | 5.13 |
| 22:30 | 2366 | Zaragoza vs Racing Santander | 1.84 | 3.16 | 4.35 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Septemba 15, 2023

Nipashe

Verratti atimkia Al Arabi UKURASA 22



Gamondi wa Yanga



Robertinho wa Simba

# Robertinho awashika pabaya Dynamos Simba ikitua Zambia

## Asema mbinu zote za wapinzani wao anazo mkononi, ameandaa mbinu...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema kuwa ana mbinu zote za wapinzani wao Power Dynamos, amezifanyia kazi na wapo tayari kwa mchezo wa kesho.

**Kauli hiyo ya Robertinho ameitoa wakati kikosi cha Simba kikiwasili salama Ndola, Zambia tayari kwa mchezo huo wa kusaka tiketi ya kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Akizungumza baada ya kutua nchini humo, Robertinho amesema baada ya kuwasoma wapinzani wao wamegundua kuwa wana wachezaji hatari wawili, mshambuliaji mmoja na kiungo, lakini pia wanapenda kushambulia kutumia upande wa kushoto.

"Nimewasoma wapinzani wetu wana wachezaji wazuri wawili, straika mmoja na kiungo na wanatumia sana kushambulia upande wa kushoto, nimetengeneza vizuri kikosi changu kwa ajili ya kuwabana sehemu yao yenye nguvu hasa kiungo, Simba hatuwezi kuwapa nafasi ya kuwa na mpira kwa sababu hiyo ni muhimu sana kwetu, usisahau pia wachezaji wetu wana vipaji vikubwa vya soka, hivyo nimewaambia wavitumie, watumie pia na mbinu zangu nilizowapa," alisema kocha huyo wa zamani wa Vipers.

Kuhusu maandalizi na hali ya kikosi alisema wachezaji wake wako kwenye hali nzuri na wanasubiri mchezo tu.

"Tumejiandaa vizuri, tuna mipango mizuri kuhusu mechi hii, kila mchezaji ana furaha na yuko tayari kwa ajili ya mechi kwa sababu malengo yetu ni kupata matokeo mazuri kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika, najua itakuwa mechi ngumu sababu tunacheza ugenini, siku zote ukicheza nje si sawa na nyumbani, pamoja na hayo nina imani na wachezaji wangu, nafikiri tutacheza vyema sana kwa sababu tuna wachezaji wenye uzoefu, tutakuwa na mashabiki wetu hapa ambao wamesafiri kuja huku kutupa sapoti," alisema Robertinho.

Juzi msafara wa mashabiki wakiwa kwenye mabasi makubwa walianza safari kuelekea Ndola ambapo wanatarajiwa kuwasili leo usiku.

Meneja habari na Mawasiliano wa klabu hiyo Ahmed Ally alikuwa miongoni mwa mashabiki waliondoka nchini juzi kwa basi kuelekea Ndola.

"Yapo zaidi ya mabasi matatu makubwa ambayo yamebeba mashabiki wa mnyama kuelekea Ndola, lakini kuna mabasi madogo madogo yapo

INAENDELEA UKURASA 23

## Gamondi awafungia kazi nyota nane Al Merrikh

**Na Saada Akida**

HUKU kikosi cha Yanga kikiwasili salama jana jijini Kigali tayari kwa mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merrikh, kocha wa timu hiyo, Miguel Gamondi amesema mchezo wa kombe la Afcon kati ya Sudan na Jamhuri ya Kongo (DRC) uliochezwa Septemba 9 umemuongezea kitu katika kuwafahamu zaidi wachezaji wa wapinzani wao hao.

Miguel aliuangalia mchezo huo na kuwafuatilia wachezaji nane wa timu hiyo waliotoka kwenye kikosi cha Al Merrikh watakaocheza nao kesho.

Kwenye kikosi hicho cha Sudan, kilikuwa na wachezaji nane wa kikosi cha kwanza chaAl Merrikh na kocha Gamondi amewafuatilia wachezaji hao.

Gamondi, alisema amewaona nyota hao na tayari amewapa maelekezo wachezaji wake namna ya kukabiliana nao kesho.

"Niliutazama ule mchezo baada ya kujua ina wachezaji wa Al Merrikh, wapo wachezaji nane na nimewaangalia kwa wale waliopata nafasi ya kucheza..., hii imeniongezea mbinu namna ya kukabiliana nao na nimetoa maelekezo kwa wachezaji wangu namna ya kucheza nao..., ni wachezaji wazuri," alisema Gamondi.

Mastaa wa Al Merrikh walicheza kwenye mchezo wa Sudan na DRC ni Mohamed Mustafa, Ramadan Agab, Bakhit Khamis na beki wa kati Mohamed Karshoum aliyecheza sambamba na beki wa Al Hilal, Mohamed Ahmed.

Wengine ni Ahmed Mahmoud na Mohamed Shambaly ambaye alitokea benchi na kati ya mastaa hao wenye uhakika wa kuanza kwenye kikosi cha kwanza kwenye mchezo wa kesho dhidi ya Yanga ni golikipa Mustapha, kiungo Agab, beki wa kati Kashroum na mshambuliaji Shambaly.

"Nilikuwa naangalia namna wanavyocheza na ubora wao,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >